# *Muungano Usioonekana Wa Bibi-Arusi Wa Kristo*

Nilifutilia mbali safari ya kuwinda, kusudi nimtumikie Bwana. Kwa hiyo ni ninii . . . Tunafurahi kuwa hapa. Ninaamini, mara ya mwisho hapa, niliwaambia: kila wakati tunapokuja, kuna mtu anayekosekana. Na endapo tutarudi mwaka ujao, na Bwana akikawia, kutakuwa na mtu fulani atayekosekana.

2 Kuna mmoja, alikuwa sana, alikuwa mpenzi wangu sana wa moyoni, rohoni; huyo alikuwa ni Ndugu Lyle. Daima nilipata makaribisho, nilipokuwa nikiingia, nikisimama nyuma kule na kusikiliza, katika chumba cha kusomea cha Ndugu Jack, ile kwaya ya zamani ya watu wanne ikiimba. Wanaimba huko Utukufuni, usiku wa leo. Vema, tayari kuna moja ya sauti hizo iliyoko Huko, ikizingojea hizo zingine tatu. Nadhani kamwe sitaisikia tena hapa duniani. Lakini kwa hakika ninatarajia kuisikia hiyo tena, Ndugu, Dada Moore hapa, katika Nchi ile ambako wataninii . . . haitazimika kamwe.

3 Ndugu Palmer alikuwa ni mtumishi mashuhuri wa Kristo. Ninaweza kukumbuka ndugu Jack akiniambia juu ya ninii yake—maisha yake yaliyowekwa wakfu kwa Mungu. Walikuwa maseremala, pamoja. Naye alisema angekuwa akila ninii chake—chakula chake cha mchana, akiwa ameshika sambusa yake mkononi, akila sambusa na huku anasoma Biblia yake. Mnaona? Alifanya mambo fulani makubwa mno, Ndugu Palmer alifanya. Yeye ni seremala mzuri, baba mzuri kwa watoto wake, familia yenye upendo. Aliwalea wote wapate kumtumikia Bwana. Kadiri nijuavyo mimi, wote wameokoka na wamejazwa na Roho Mtakatifu. Na huo ni mchango mkubwa kwa mwanamume yeyote siku hizi, wavulana kwa wasichana. Lakini, unaona, yote yale aliyowahi kufanya hayatakuwa na maana sana mpaka amtumikie Mungu, asipomtumikia Mungu. Na usiku wa leo, yale aliyokuwa amefanya hapa duniani, matendo yake mema, ameenda kupata thawabu yake, kuwa pamoja nao. Mungu na apumzishe nafsi ya ndugu yetu.

4 Ninajua, ilimradi hii ni maskani hapa, nami ni—ninajua yeye ataninii . . . sauti yake ingali itakuwa hapa. Unaweza kuisikia. Dada Anna Jeanne na—na dada yake, wakipiga kinanda na piano, jinsi ambavyo haikuwabidi kamwe kusubiri. Ndugu Palmer anasimama tu hapa na kuchagua tu wimbo, na kuendelea. Wao wangeushika. Nami kamwe . . . Nilitazamia kumsikia akiongoza wimbo.

5 Kwa watoto wake; kwa mke wake; na kwa Ndugu Jack, rafiki yake msiri, wamekuwa marafiki kwa miaka hii yote; na Ndugu Brown, Dada Brown, na ninyi nyote wa maskanini; Mungu awabariki. Namkumbuka kwa huzuni, pia. Mungu na aipumzishe nafsi yake shujaa, hata tutakapokutana naye katika amani.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

6 Baba wa Mbinguni mwenye rehema, nikizungumza tu juu ya mtumishi huyu mashuhuri, nilimkumbuka kwa masikitiko, usiku wa leo, yeye tukipeana mikono, na tabasamu hilo la kuvutia sana alilokuwa nalo daima aliposema, "Mungu akubariki, Ndugu Branham," wakati tukienda kuingia mlangoni. Ninajua amepanda kuja Nyumbani Kwako, usiku wa leo. Kwa hiyo ninaomba, Mungu mpenzi, ya kwamba utajalia matunda, kazi zake zinazomfuata, zitukuke, zikiendelezwa na watoto wake, mke wake. Tunaomba kwamba utambariki, Bwana. Ulisema ungekuwa mume kwa "wajane walio wajane wa kweli." Ninamwombea Dada yetu Palmer na watoto wote. Ninajua kuhurumia pande zote mbili, kumpoteza mwenzi na pia kumpoteza baba yangu.

7 Kwa hiyo, Baba, wakati tukiwa hapa, usiku wa leo, tunaomba ya kwamba utaitayarisha mioyo yetu, pia, kwa ajili ya saa hiyo. Hatujui. Inaweza ikaja kwa ghafla tu kama yake ilivyokuja. Hatujui itakuja lini, bali tunajua haina budi kuja. Kwa hiyo tunaomba, Mungu, ya kwamba utauchunguza kila moyo uliomo humu ndani, usiku wa leo. Mungu, usiuache wangu. Uchunguze wangu, pia, na unihakikishe. Bwana, kama kukiwepo na uovu wowote ndani yetu, uondoe. Tunataka kukutumikia. Hilo ndilo lengo letu kamili, ni kukutumikia Wewe.

8 Tumiminiie Roho Yako, usiku huu, na siku zilizosalia za juma hili. Ibariki maskani hii inayoitwa kwa jina la Maskani ya Uzima. Jalia ipokee baraka kamili za jina hilo na ijae Uzima wa Mungu, juma hili, ipate kuokoa kila nafsi iliyopotea, ipate kumjaza kila mwaminio kwa Roho Mtakatifu, na kufanya upya matumaini yaliyo ndani yetu, Bwana, tena. Tunaomba ya kwamba Wewe utawaponya pia wagonjwa wote na wanaoteseka wanaokuja miongoni mwetu. Jalia Roho Wako Mtakatifu mkuu awe hapa, Bwana, na aponye tu. Pia amtie mafuta kila mtu apate kuamini. Tujalie mambo haya, Baba.

9 Mungu, nisaidie sasa. Kama ikiwadia, zamu yangu ya kuuleta Ujumbe imewadia. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utaifanya sehemu ya kibinadamu isimame kando. Roho Mtakatifu na aingie na atende kazi miongoni mwetu, Bwana. Roho Mtakatifu na autwae mkutano, Bwana. Tunajua ya kwamba tu wapungufu mno. Tusingeweza kufanya jambo hilo, hata mmoja wetu. Hatudai kuwa na uwezo wa kufanya jambo

hilo. Lakini, Bwana, tunajua ya kwamba Wewe Ndiwe mwenye uwezo. Kwa hiyo tunakutegemea Wewe, Bwana. Tembea, Roho wa Mungu, na utushukie upya. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

10 Sasa, nataka kutoa salamu moja baada ya nyingine, kwa makanisa sasa yaliyo kwenye mtandao huu wa simu kote nchini. Tuko kwenye mtandao wa simu, ambao ni mfumo mdogo mzuri ambao tumeweza kupata, kupitia kwa Ndugu yetu Pearry Green kutoka Beaumont, Texas. Na hayo makanisa, yote, yanayofuata Ujumbe huu, kote katika Marekani, yameunganishwa kwa simu, usiku huu. Tunatuma salamu, huku na huko kwenye Pwani ya Magharibi, kote kote kushuka kutoka Vancouver mpaka Tijuana, Mexico, kupitia San Jose, Los Angeles. Makundi yote yaliyoko kule, tunawasalimu kutoka Shreveport. Pia, kote mpaka Prescott, Arizona, kwa kundi lililoko kule ambalo linamngojea Bwana, tunawatumia salamu, na huko Tucson, pia Sierra Vista. Kote kote mpaka New York, huku na huko, kote nchini, Bwana awabariki, kila mmoja. Laiti mngalikuwa hapa, usiku wa leo, jimbo hili zuri la zamani la Louisiana, ambalo linaonekana kana kwamba ni makazi ya pili, kwangu mimi. Ni-. . .

11 Mnajua, ninyi watu mlioko huko New York, nyote kwa namna fulani tunawachekelea kidogo, jinsi mnavyoongea. Niko nyumbani kabisa usiku huu. Naam. Kila mtu huku tuliko, mwajua, walisema, "Aloo, mbendwa, Ndugu Branham. Umemleta Dada Branham na wadodo wode na ukaja hapa kutuona." Loo, jamani! Hilo linanifanya nijisikie vizuri. Hicho ni Kiingereza halisi, kwangu mimi. Si kuwadharau ninyi watu mnaoishi mashariki na kaskazini, na sehemu mbalimbali. Lakini, mnajua, nadhani nilizaliwa maskini Mwasi wa kale tu na inanibidi kudumu hivyo. Kwa namna fulani na—nakipenda, mimi mwenyewe. Ni Kiingereza halisi.

12 Nilikuwa kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, hapa si muda mrefu uliopita, nao wakasema, "Sasa tutasimama na kuimba wimbo wa taifa." Ndipo nikasimama, nikasema, "Nayapenda maskini makazi yangu ya kale ya Kentucky, mbali sana." Vema, kwangu mimi, huo ulikuwa ndio wimbo wa taifa. Hayo ndiyo tu niliyojua kuhusu hilo. Kwa hiyo, tunawapelekeeni salamu. Na sasa kwa nanii . . .

13 Ninaamini watajaribu kutangaza hicho kiamshakinywa, pia, kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, Jumamosi asubuhi. Ndugu Green atawaambia, kwa kuwa yeye yuko kwenye vipaza sauti huko nje sasa. Kwa hiyo atawaambia kiamshakinywa kitaanza saa ngapi, na ni saa ngapi, kila usiku, mtafungulia redio zenu. Tunawashukuru kwa ukarimu sana. Tuombeeni.

14 Sasa, kwa kusanyiko la mahali hapa, na maskani ya Ndugu Jack, nitawaomba tu idhini, usiku wa leo. Kwa kuwa nilikuwa

ninataka kutoa Ujumbe wangu wa kutoa shukrani kote n—nchini, usiku huu, kwa makanisa yetu ya humu nchini yanayoutii Ujumbe. Katika jambo hili, i—inawezekana nikachukua muda mrefu kidogo. Na halafu, tena, huenda nikahubiri Fundisho fulani. Kwa hiyo, kama ndiyo hivyo, na hukubaliani Nalo . . .

15 Kama tu nilivyosema sikuzote kuhusu kula sambusa ya tunda la cheri: "Ninapoifikia mbegu, siitupi hiyo sambusa, ninatupa hiyo mbegu, ninaendelea tu kula sambusa."

16 Kwa hiyo kama ikitokea kwamba nitaje jambo fulani usiku wa leo, mimi-. . . Vema hiyo ndiyo sababu moja iliyonifanya kuitikia mwaliko huu, usiku wa leo, kuwa hapa, kuyaletea makundi mbalimbali kote nchini Ujumbe wangu wa kutoa shukrani, ilikuwa ni kwa sababu Ndugu Jack yuko huru sana sikuzote kufungua mlango wake na husema, "Hubiri kilichoko moyoni mwako." Kwa hiyo ninajisikia nyumbani kabisa.

17 Kwa hiyo inawezekana ya kwamba humu ndani, katika kusanyiko la mahali hapa la Ndugu Jack, huenda kukawa kuna wahudumu wengine na baadhi ya watu ambao wasingekubaliana na Fundisho. Kwa kawaida ninaheshimu kutotaja fundisho kwenye mimbara ya mtu, ambaye amenialika nije nikamsaidie kuhubiri. Kwa hiyo, baada ya usiku wa leo, nadhani nitakuwa tu nikiwaombea wagonjwa na kufanya ibada ya kawaida. Lakini nilifikiria ningewajulisheni kabla, ya kwamba kama nikisema kitu ambacho huenda kisikubalike, mbona, kihesabu tu kwamba ni kwa ajili ya ujinga wangu, nadhani, wala sijui vema zaidi. Na mniombee.

18 Kwa hiyo sasa hebu na tufungue kwenye Neno, kwenye mlango fulani hapa. Ninataka kurejea sehemu nyingi usiku wa leo, kwa maana nina Maandiko mengi na mihitasari midogo iliyoandikwa hapa kwenye padi.

19 Ninakumbuka mara ya kwanza nilipopanda jukwaani kwenye Maskani ya Uzima, miaka ishirini iliyopita. Ha—haikunibidi kuandika Maandiko yangu na marejeo. Nilikuwa tu na umri mdogo zaidi kwa miaka ishirini wakati huo. Bali sasa nimekwisha kupita umri wa miaka ishirini na mitano, kwa hiyo mimi . . . kwa mara ya pili. Kwa hiyo nimeninii . . . siwezi kuyakumbuka kama nilivyokuwa nikiyakumbuka. Inanibidi kuandika Maandiko yangu, na mara nyingine niandike kitu chochote kwa ufupi ninachotaka kukirejea.

20 Na sasa Bwana na abariki tunaposoma kutoka kwenye Neno la Mungu, na Kitabu cha Warumi, mlango wa 7. Sasa, ninataka kwa namna fulani kufundisha jambo hili kama somo la shule ya Jumapili.

21 Ninajua kuna watu ambao wamesimama. Na kule maskanini, kwa kawaida, kule Jeffersonville, tunataka kuwasalimu ninyi nyote, usiku wa leo, pia, tukijua ya kwamba mko kwenye mtandao huu huko maskanini. Na inaonekana

kana kwamba mkiwa huko maskanini, usiku wa leo, kama mngelikuwa huku, watu wakiwa kandokando ya kuta, na wamefurika. Sasa, ninadhani mko hivyo, pia, watu wote mlio kwenye sehemu hiyo ya nchi, ambao mmekuja kwa ajili ya Ujumbe.

22 Sasa tutatumia hili kama somo la shule ya Jumapili. Wala halijaelekezwa kwenye kitu chochote, kwa watu wowote, wala chochote kile; ni kwa Kanisa tu, Mwili wa Kristo ambao tunajaribu kuuongoza kwenye mawazo ya kilindi na makusudi ya juu zaidi, tukiamini ya kwamba Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia. Tunaamini jambo hilo. Zaidi sana, kumekaribia kwa miaka ishirini zaidi kuliko ilivyokuwa mara ya kwanza nilipokuja Shreveport. Loo, mambo mengi sana yametendeka tangu wakati huo! Sasa tunakutazamia Kuja kwa Bwana, katika kizazi chetu. Sitazamii uamsho katika kizazi chetu. Ninakutazamia Kuja kwa Bwana, katika kizazi chetu.

23 Sasa katika Warumi 7. Nikiamini ya kwamba mmefungua Biblia zenu, kila mahali sasa, kote nchini. Tunataka kusoma kwa makini sasa. Huu—huu Ujumbe unaotolewa hapa, unaonekana kana kwamba ni juu ya ndoa na talaka, bali kwa kweli sivyo. Kwangu mimi, ni unabii kwa ajili ya Kanisa katika siku za mwisho. Na tusome.

> *Ndugu zangu, hamjui, (maana nasema na hao waijuao sheria), ya kuwa torati humtawala mtu wakati anapokuwa yu hai?*
>
> *Kwa maana mwanamke* aliye *na mume amefungwa na sheria kwa yule mume wakati anapokuwa yu hai; bali akifa yule mume, amefunguliwa ile sheria ya mume.*
>
> *Basi wakati awapo hai mumewe, kama* akiwa *na mume mwingine huitwa mzinzi: ila mumewe akifa, amekuwa huru, hafungwi na sheria hiyo, hata yeye si mzinzi, ajapoolewa na mume mwingine.*
>
> *Kadhalika, ndugu zangu, ninyi pia mmeifia torati, kwa njia ya mwili wa Kristo, mpate* kuunganishwa ama mpate *kuolewa na mwingine, yeye aliyefufuka katika wafu, kusudi tumzalie Mungu matunda.*
>
> *Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata tukaizalia mauti mazao.*
>
> *Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko.*

24 Na sasa hebu tuombe.

25 Mungu mpenzi, ndio kwanza tusome lile tunaloamini kuwa ni Neno takatifu la Mungu. Na hilo ndilo tunaloamini, kwamba hakuna yodi moja wala nukta itakayopita kamwe kutoka

kwenye Hili mpaka yote yatakapotimizwa. Nasi tunaamini ya kwamba Bwana wetu alitwambia, katika Ufunuo mlango wa 22, ya kwamba, "Mtu yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka Kwake ama kuongeza neno moja Kwake, huyo, sehemu yake, itaondolewa katika Kitabu cha Uzima."

26 Nasi tunaona ya kwamba, kwa kufasiri Neno hili vibaya, kama vile Shetani alivyolifasiri vibaya kwa Hawa, kulimfanya ashuku Neno moja, kukaitupilia jamii yote ya binadamu katika machafuko ya anguko. Neno moja tu!

27 Kisha tunaona katikati ya kile Kitabu, alikuja Bwana na Mwokozi wetu, naye alitupa nukuu hii kuhusu jambo Hilo. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

28 Halafu lile onyo kali katika Kitabu cha mwisho, cha Ufunuo wa Yesu Kristo, "Yeyote atakayeongeza neno moja ama kuondoa Neno moja, ataondolewa sehemu yake katika Kitabu cha Uzima."

29 Ee Mungu, tukijua, tukiona jinsi tulivyo wadhaifu, tukijua ya kwamba tunatembea juu ya nyuzi dhaifu za maisha, za maisha haya yasiyodumu (tukiwa hatujui ni wakati gani tutakapoitwa kwenda kujibu huko Juu), tujalie, Ee Bwana, tuweke kando kila kitu moyoni mwetu, kila kitu niani mwetu, na tuangalie moja kwa moja kwenye Neno Lako, usiku wa leo, na tukutazamie Wewe uje na kulifasiri kwa mausia matakatifu. Tujalie hayo.

30 Twaomba Roho Wako atushukie na kulitia Neno mafuta moyoni mwetu, tupate kuondoka hapa, jioni ya leo, watu bora zaidi kuliko tulivyo sasa, tupate kumfahamu Yesu Kristo kwa undani zaidi. Tujalie hayo, Bwana, tupate kuifahamu siku tunayoishi, na matayarisho ya Mungu kwa ajili ya watu Wake katika saa hii; wakati huu mkuu, muhimu sana na wenye giza tunaoishi sasa. Mungu, tutie mafuta, si mnenaji tu, bali na msikilizaji. Na, sote pamoja, ifanye mioyo yetu itetemeke mbele za Neno Lako. "Kwa kuwa kumcha Mungu ndio mwanzo wa maarifa." Tujalie mambo haya, Baba, kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

31 Ningependa kuyapa kichwa matamshi haya machache ambayo nilikuwa niyazungumze hapa, na Maandiko fulani ambayo ningetaka kuyafuatilia nyuma kwa makini, Bwana akipenda, kwa—kwa ajili ya Ujumbe wa kutoa shukrani, kwa usioonekana, wa: *Muungano Usioonekana Wa Bibi-Arusi Wa Kristo*. *Muungano Usioonekana Wa Bibi-Arusi Wa Kristo*. Hausikiki kama ni Ujumbe wa kutoa shukrani. Hata hivyo, Andiko lolote, tunashukuru kwa ajili ya Hilo lote.

32 Ninamshukuru Mungu, kuishi katika wakati huu, wa matukio ya kumalizia historia ya ulimwengu huu. Sijui. Kama ningalikuwa na la kusema kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na Mungu awe ameniwekea wazi mpango wote, na

kuniambia, "Na—nataka wewe uhubiri. Basi sasa ni wakati upi ungetamani, kwenda duniani ukahubiri?" Ningalichagua wakati huu, kwa maana ninafikiri hiki ndicho kipindi cha heri na furaha kubwa.

33 Hakika ningalipenda kuwa hapa wakati wa ziara Yake duniani. Lakini, hata hivyo, nafikiri huu hapa sasa ndio wakati mkuu zaidi, kwa maana ndio wakati anaokuja kuwachukua watu ambao amewakomboa, tunapokaribia ufufuo ambapo wote waliokombolewa watafufuka. Ni nafasi ya fahari jinsi gani tuliyo nayo, kuwahubiria watu wanaokufa, ni wakati mkuu mno! Tunaufurahia sana.

34 Na tunajua ya kwamba historia inafikia mwisho wake. Historia ya ulimwengu itakwisha hivi karibuni, ndipo tutaingia kwenye siku mpya, kwenye ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu. Huo, kama mwaminio mmoja, ninaamini katika ninii . . . katika Utawala wa Miaka Elfu, Utawala wa Miaka Elfu pamoja na Kristo, miaka elfu moja duniani; kule kurudi kwa Bwana Yesu katika mwili, kuwachukua watu wenye mwili, uliotukuzwa, kwa Damu Yake inayosafisha.

35 Paulo hapa anaeleza kwa mfano, katika Maandiko yetu, kuhusu torati na neema, na kulielezea kwa mfano kama ndoa na talaka. Fungu hili ni mara chache sana linahubiriwa, kwa sababu liko ninii, kwa namna fulani, linahusu, kitu kama, ndoa na talaka. Lakini pia linahusu sehemu kubwa zaidi ya ndoa na talaka, kuhusu jinsi ambavyo yeye anajaribu kuweka katika utaratibu hapa ya kwamba sisi, kama ninii—kama Kanisa, haiwezekani tena tuwe tumeolewa na dunia na Kristo pia, wakati uo huo, na—na liwe ni jambo la haki na halali, kama vile isivyowezekana kwa mwanamke kuwa anaishi na mume mwingine wakati yeye ana mume aliye hai. Nami nina mawazo yangu mwenyewe juu ya jambo hilo, nami ninaamini ya kwamba yale Biblia isemayo ni Kweli.

36 Sasa, bali ninaamini, pia, ndivyo ninavyoamini, ya kwamba jambo hilo linafungua moja ya siri kuu za unabii. Nami ninatumaini ya kwamba Bwana atatusaidia, usiku wa leo, tunapouhubiri huu kwa watu wetu wanaongojea kote nchini.

37 Ilisemwa, wakati mmoja (nilikuwa nikisoma, wakati nilipokuwa nikiandika muhtasari wa jambo hili, ni—nisingeweza kukumbuka liko kwenye kitabu kipi hasa, lakini ni—nina hakika hili ni kweli), ya kwamba (moja ya vitabu nilivyosoma juu ya Bw. Moody, Dwight Moody, huko Chicago; tuna kanisa lenye usikivu mkubwa huko Chicago, pia, usiku wa leo), ya kwamba, Bw. Moody, baada ya kusoma Warumi 7, alikimbilia mtaani, na mtu wa kwanza aliyekutana naye, alimwambia, "Je! unajua neema?"

Ndipo huyo mtu akajibu, "Neema nani?"

Bw. Moody akajibu, "Neema ya Mungu."

38 Kwa hiyo, ilimsisimua sana wakati alipoona vile, jinsi neema ilivyokuwa imetutenganisha na torati, na jinsi, kwamba ni kazi gani neema ilifanya. Vema, sasa, lolote ninalotaka kufanya, ni wakati. . . Daima niliwaambia watu, nitakapovuka ule mstari, Ng'ambo ya pili, ningependa kusimama na kuimba.

> Neema ya ajabu! Jinsi inavyosikika tamu,
> Iliyomwokoa mnyonge kama mimi!
> Neema, neema ya thamani!
> Laiti ningalijua neema nyingi zaidi!

39 "Kwa maana tunaokolewa kwa neema; si kwa yale tunayoweza kufanya." Tunayoweza, lolote tufanyalo, halihesabiwi kwetu. Neema ndiyo inayotuokoa. "Mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani."

40 Hebu niongezee kwa Mwanamke huyu, Neema, hebu nimweke kwenye Biblia, pia, anavyoitwa Bibi mteule, huyu Binti Neema nitakayenena habari zake. Ujue, Biblia inatangaza, ilisema, "Kwa Bibi mteule." Hilo, kama ukiangalia, "mteule" linatokana na neno "Bibi aliyeteuliwa." Bibi mmoja, miongoni mwa mabibi wengine wote, aliteuliwa.

41 Kama vile, yule bikira alikuwa auzae mwili wa Mungu, duniani. Alikuwa ni mwanamke aliyeteuliwa. Mungu alimchagua Mariamu.

42 Na, pia, Mungu amemchagua Bibi mteule, ambaye ni Bibi-arusi Wake. Yeye ameteuliwa. Ninatumaini sisi ni washiriki wa huyo, usiku wa leo, kote duniani, kote nchini, hasa.

43 Kielezo chake hapa, kikionyesha uhusiano wa Bibi-arusi na Kristo, Bibi mteule: na jinsi alivyopaswa kuletwa Kwake; mahali ambako angetoka; na jinsi ambavyo angeletwa Kwake. Kanisa hapa, katika kielezo tulicho nacho mbele zetu, linafananishwa na mwanamke. Ambapo, mwanamke sikuzote ni mfano wa Kanisa, kwa maana kanisa linahesabiwa kwamba ni Bibi-arusi. Bibi-arusi, Yeye ni Bibi-arusi wa Bwana Yesu, Mwana wa Mungu.

44 Daima, kama utachunguza, uchunguze hali na mienendo ya wanawake, basi utaona mahali kanisa lilipo.

45 Sasa, hili, baadhi ya matamshi haya huenda yakaonekana ni mageni kwa wengine wenu, bali yanathibitisha Ujumbe nilio nao kutoka kwa Bwana, ambao ninajitahidi kuwafikishia watu. Unaona? Hebu angalia kila kitu katika hali yake ya asili, jinsi yanavyokuwa, maumbile, na uyachunguze. Yanaambatana kihakika na mambo ya kiroho, pia.

46 Sasa, kama utachunguza mienendo ya wanawake ulimwenguni leo, chunguza mwenendo wa kanisa la kilimwengu leo. Chunguza tu. Bila shaka, sasa, pia kuna mwenendo wa Bibi–arusi wa kiroho pia, lile Kanisa. Unaona? Chunguza jambo

Hilo, pia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Kwa sababu, hilo linaloitwa la kawaida, linadai kuwa ndilo Bibi-arusi.

47 Sasa, naomba kuliambia tena kusanyiko la mahali hapa. Msijisikie vibaya sasa. Ni—ninawazungumzia wote kote nchini, kwa ninii, wale ninaowadhania, ndio Bibi mteule. Kwa hiyo ikitokea kuwepo na wahudumu humu ndani, ambao hawakubaliani na hayo, vema, hebu tulieni tu kwa kitambo kidogo. Mnaona? Angalieni. Hebu sikilizeni tu.

48 Angalieni tabia hii. Unapowaona wanawake wakipotoka tu, wakifanya tu jambo lolote wanalotaka kufanya, angalia, kanisa linafanya jambo lile lile. Angalia.

49 Bali angalia wakati, yule Bibi-arusi wa Kiroho, wakati atakapoanza kuwa na uamsho, wakati atakapoanza kurudi na kujiweka sawa na Neno la Mungu. Basi angalia tena, unaona, jinsi Maandiko yalivyo, wakati huo, kutakuwako na Ujumbe utakaosambaa haraka wa kumshika huyo Bibi-arusi, kumshika huyo Mwanamke, Mteule.

50 Kwa kuwa, ni kama vile ulimwengu, Shetani, yule mdanganyifu aliyemdanganya yule bibi-arusi wa kwanza, kufanya dhambi dhidi ya Mungu, kwa kutoliamini Neno Lake. . .

51 Na sasa, leo hii, tunapoona kanisa la kawaida, katika injili yenu ya kiakili, likizidi kwenda mbali zaidi na zaidi na Neno, katika injili ya kirafiki; tunaona ya kwamba wanawake wa ulimwengu, huko mitaani, wafuasi wa hilo, wanafanya mabaya katika mazingira yale yale. Huwezi kuwaambia. Wamepoteza hisia zote za uadilifu wa kawaida, hao watu wamezipoteza. Mnaona? Na hivyo ndivyo kanisa limefanya. Nawe unaweza kuliona likienda moja kwa moja kwenye baraza la ekumeni, kwa hakika tu kama kitu chochote kile ulimwenguni, na kuingia moja kwa moja Rumi upesi sana liwezavyo kwenda, unaona, kwa maana imetabiriwa. Na huyo hapo. Hiyo ndiyo tabia yake.

52 Lakini basi angalia tena kwenye Kanisa la kiroho, jinsi ambavyo kundi hilo la watu, walioitwa watoke, Wateule, kupitia kwenye kila uamsho. Wakati wa Martin Luther, ilitukia vivyo hivyo katika yale matengenezo. Ilitukia vivyo hivyo wakati wa John Wesley. Ilitukia vivyo hivyo wakati Upentekoste ulipoanza kwa mara ya kwanza. Waliwarejesha hao wanawake moja kwa moja katika Neno, kisha wakaliacha. Huyo hapo akirudi moja kwa moja kwenye machafuko. Lakini basi wakati ambapo watu wanapokuwa tayari kujiweka sawa, kuna Ujumbe unaotokea, nao wanajiweka sawa Nao.

53 Luther alikuwa mjumbe wa siku moja, ya kuhesabiwa haki, nalo Kanisa likajiweka sawa moja kwa moja na huo, baadhi yao. Hao wengine wakaendelea. Wesley akaja na utakaso, Kanisa likajiweka sawa nao. Pentekoste ikaja na kurudishwa kwa vipawa, Kanisa likajiweka sawa moja kwa moja nao, wale

Wateule wa siku hiyo; na kisha wakafifia, wakarejea moja kwa moja kwenye umadhehebu na wakaondoka moja kwa moja pamoja na hao wengine, wote hao moja kwa moja kwenye mwelekeo uo huo.

54 Sasa, lakini unaona, wakati watu wanapoanza kujitahidi kujiweka sawa na Neno, kunakuja Ujumbe mpya kutoka kwenye Neno la Mungu, kuwaendea watu hao moja kwa moja. Nao wanaukamata Ujumbe huo na kujiweka sawa, kila wakati. Liko tu katika ninii ya Mungu . . . Tuna mambo hayo.

55 Tunazo familia. Kila familia hapa ndani imezoea jambo hilo. Wakati mwingine kila kitu kitakuendea vizuri, kwa miaka kadhaa. Kisha, mara, utafikia kipindi ambacho, tunasema hilo mara nyingi huku Kusini, "Hakuna msiba usiokuwa na mwenziwe," na kila kitu kinavurugika. Unapitia katika kipindi cha usiku. Ndipo kunapambazuka, kisha kipindi cha usiku. Kila kitu kinakwenda katika mwendeleo wa moja kwa moja.

56 Nabii, Paulo, hapa anasema ya kwamba mwanamke hawezi kuolewa mara ya pili mpaka mume wake wa kwanza amekufa. Hawezi kuolewa tena mradi tu mume wake wa kwanza angali hai; yeye, hawezi kwa hali yoyote ile, kamwe. Inamlazimu kubaki pasipo mwenzi mradi tu mume wake wa kwanza yu hai. Na kama akitenda dhambi kama hiyo, "ataitwa mzinzi." Ninazungumza juu ya mambo ya kawaida sasa, kuyafananisha na ya kiroho. Kama mwanamke huyu angetenda dhambi kama hiyo, basi anatiwa alama, "mwanamke mzinzi," endapo ana wanaume wawili walio hai kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, yeye amepoteza, kwa kufanya jambo hili, haki zake kwa Mungu na Mbinguni, kwa kufanya jambo hilo. Hakika amepoteza. Yeye ametupiliwa mbali na mpango wa Mungu, kwa mujibu wa Maandiko ambayo nimekwisha yasoma sasa hivi.

57 Vivyo hivyo na kanisa, linapojaribu kuchanganya kanuni za imani na madhehebu pamoja na Neno la Mungu. Haliwezi kuolewa na madhehebu, na liwe Bibi-arusi wa Kristo, kwa wakati mmoja. Sharti liwe limemfia mmoja au mwingine. Ndivyo inavyosema torati, hapa. Kuna sheria nyingi sana katika Neno la Mungu. Na hiyo ni sheria Yake, Paulo akizungumzia jambo lile lile hapa. Haliwezi kuolewa na kanisa la kanuni za imani za kilimwengu, na liwe Bibi-arusi wa Kristo, kwa maana (hilo) moja linapinga lingine. Sasa, kumbuka.

Mnasema, "Vema, tunaamini *hili*, bali hatuamini *Lile*."

58 Kama umeolewa na Kristo, Kristo ni Neno la Mungu. Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 1, ulisema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Na yuyo huyo alifanyika mwili akakaa kwetu." Kristo alikuwa ndiye Neno lililo hai. Yeye daima alikuwa ni Neno. Angali ni Neno. Daima atakuwa ni Neno. Yeye alikuwa

tu ni dhihirisho la sifa za Mungu, kwa kuwa alikuwa ni Mwana wa Mungu.

59 Na mwana yeyote ni sifa za babaye, na jinsi tu vile wewe ulivyokuwa katika jeni za baba yako, katika mwili wa baba yako alipokuwa mvulana mdogo, ulikuwa ndani yake. Hata hivyo, yeye asingeweza kuwa na ushirika na wewe, kwa sababu hakukujua. Lakini basi, kupitia kwenye tumbo la uzazi la mama, ulizaliwa duniani na ukachukua sura ya baba yako, ndipo angeweza kufanya ushirika na wewe.

60 Na ndivyo mlivyokuwa, wana wa Mungu na binti za Mungu, kabla hata hakujakuwa na mwezi, nyota, ama molekuli. Mlikuwa wana na binti za Mungu, kwa kuwa ninyi ni onyesho tu la kimwili la sifa zilizokuwa ndani ya Mungu hapo mwanzo. Kwa kuwa, kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ulikuwa ni wewe, hapo awali. Hujui lolote kuhusu hilo. Wala hukujua wakati ulipokuwa ndani ya baba yako wa duniani, lakini umedhihirishwa, pia, katika sura yake. Umefanywa katika sura ya Mungu, nawe ulidhihirishwa kwa ajili ya utukufu na ushirika wa Mungu.

61 Na, hivyo basi, kwa hakika tu kama vile jeni yako ilivyopaswa kuwa ndani ya baba yako, kabla ya kuzaliwa kwako kwa kawaida, ilibidi jeni yako ya kiroho iwe ndani ya Mungu, kwa kuwa wewe ni dhihirisho la sifa za mawazo Yake, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Vema. Hakuna njia ya kulikwepa. Hiyo ni kweli. Sasa, sasa tunaona, basi, huo Uzima ukiwa ndani yako, Uzima wa Mungu ukiwa ndani yako, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

62 Sasa, sasa, huwezi kuchanganya kanuni za imani za madhehebu pamoja na Neno, kwa maana zinatofautiana sana, moja na lingine.

63 Hivyo ndivyo hasa Shetani alivyojaribu kufanya na mawazo yake ya kiakili kwa Hawa. Alisema alikubali ya kwamba Mungu alisema jambo hilo, lakini akasema, "Hakika, hamtakufa." Unaona? Nao wanaamini hilo.

64 Na hivyo ndivyo kanuni za imani zimefanya, usiku wa leo. Madhehebu yamewatenganisha watu na Neno la Mungu. Je! Yesu hakusema, hapo alipokuja, "Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmetangua Amri za Mungu kwa watu"? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Na kwa kanuni zetu za imani, tumetenganisha ushirika wa Roho Mtakatifu kulitia mafuta Neno la Mungu lililokusudiwa kwa ajili ya kizazi hiki. Kwa namna hiyo tumewatenganisha watu, kwa madhehebu, hata hawawezi kupata nafasi ya kuona Hilo.

65 Sasa, Mungu, Yeye, kila kizazi, Yeye huongeza sehemu mpya ya Kitabu Chake. Yote yanaambatana pamoja.

66 Kama vile ambavyo mwili wangu ulivyoumbwa. Ninaambiwa ulianza kwa uti wa mgongo, bali wote haukuwa

ni uti wa mgongo. Ulitoka hapo ukawa mbavu, na kutoka kwenye mapafu, na kwenye vitengele, na mikono, na miguu, na kadhalika, ndipo ukaja kuwa mtu niliye mimi.

67 Na hivyo basi Mungu alidhihirishwa hapo mwanzo. Na hatimaye akatokea kama Yehova, Mungu Baba. Ndipo akatokea kama Mungu Mwana, katika Yesu Kristo. Sasa ametokea kama Mungu Roho Mtakatifu. Mungu yeye yule, wakati wote, madhihirisho matatu ya ninii—Mungu yeye yule.

68 Sasa, tunaona katika jambo hili, ya kwamba, kila kizazi, Mungu amelikusudia Neno Lake tangu mwanzo.

69 Ni kama tu vile mabadiliko ya polepole yalivyokuja. Ni kama tu kile kitu cha kwanza alichoumba Mungu, labda, kilikuwa . . . Hebu tuseme Yeye aliumba mimea, kwanza. Kisha akaumba wanyama, baadaye. Ndipo akaumba binadamu, baadaye. Kitu kama mabadiliko ya polepole, yakiendelea kuwa bora zaidi.

70 Ndivyo imekuwa katika Mungu na Kanisa Lake. Kuhesabiwa haki chini ya Luther. Kutaka- . . . Huko ni kumvuta Bibi-arusi Wake atoke, sasa. Yeye anamwumba Bibi-arusi Wake. Kuhesabiwa haki chini ya Luther; kutakaswa chini ya Wesley; na kadhalika, unaona. Yeye, mabadiliko ya hatua kwa hatua ya Roho yakitolewa zadi na zaidi, maana huo Mwili unajengeka, kufikia Kichwani, ambacho ni Kristo, huo Mwili wa Kristo.

71 Sasa, Yeye, kama mwanamke, kama ameolewa na Kristo aliye Neno, hawezi kuolewa na madhehebu ya kanisa kwa wakati huo huo, kwa kuwa amefungwa nayo. Ataninii . . . hawezi kuishi na hao waume wawili kwa wakati huo huo. Wanatofautiana, mmoja kwa mwingine. Moja limetumwa na Mungu, lingine limefanyizwa na mwanadamu, kwa hiyo yanahitilafiana. Alisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo; Langu na liwe Kweli." Mungu alisema hivyo.

72 Yanahitilafiana tu moja kwa lingine, kama vile torati ilivyotofautiana na neema, kama vile Paulo anavyosema hapa. Mmoja hana budi kuwa amekufa, kumpata huyo mwingine. "Na kama amejaribu kuwachanganya, ataitwa mzinzi." Loo! Wazieni jambo hilo. New York, Arizona, kote nchini, wazieni jambo hilo. Mungu alisema, "Kama akijaribu kuolewa na wawili wakati uo huo, ataitwa mzinzi." Ni mzinzi gani anayeweza kuingia Mbinguni? Je! Mungu angeweza kuoa mwanamke mzinzi? La hasha. Alituambia tusifanye jambo hilo. "Ataitwa mzinzi."

73 Basi, watoto wake, kama yeye ni mzinzi, watoto wake ni haramu. Haramu! Ni haramu kwa kitu gani? Si kwa kanisa, bali kwa Neno. Huyo ni mwanamke haramu. Ni picha ya namna gani ya hii Ufunuo 3 hapa, ya siku ya mwisho, wakati wa kanisa la Laodikia! Ni kundi haramu jinsi gani! Ni mchanganyiko wa kimadhehebu wa namna gani! Vuguvugu, wanatenda maovu na kujiita wenyewe ni Wakristo, na kulikana Neno la Mungu,

"Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake," kama nabii alivyosema wangekuwa.

74 Ndoa ndiyo desturi ya zamani sana ulimwenguni. Ndoa ilitekelezwa kwanza, na kuidhinishwa, katika bustani ya Edeni.

75 Mwanamke amewekewa amana tabia fulani ambazo hapaswi kuzichafua. Mwanamke amewekewa amana hizo. Hakuna kiumbe duniani kilicho kama mwanamke. Hakuna mbwa jike, hakuna jike la aina yoyote, lililopewa tabia ambayo mwanamke amepewa.

76 Mwanamke hata hakuwapo mwa—mwanzo wa uumbaji, kwa kuwa Mungu alijua ya kwamba angeanguka. Majike wengine wote wasingeweza kufanya uzinzi. Yeye ndiye pekee anayeweza kufanya uzinzi. Kama angalikuwa ameumbwa kama kiasili, hilo lisingekamilisha hekima kuu ya Mungu. Unaona? Yeye alifanywa zaotuka la mwanamume.

77 Lakini kwa sababu alitupwa upande huo, yeye pia amekabidhiwa dhamana takatifu kutoka kwa Mungu, kwa ajili ya ukombozi. Yeye ana sifa ambayo hapaswi kuzitia unajisi.

78 Kama akizichafua, ametiwa unajisi maishani mwake mwote. Haidhuru amesamehewa jinsi gani, hawezi kuhesabiwa haki. Nitafikia jambo hilo katika muda mfupi. Nina Maandiko juu ya jambo hilo, katika dakika chache. Anaweza kusamehewa unajisi wake, ila hawezi kuhesabiwa haki katika maisha haya. Analo daima. Angalia sasa. Amekabidhiwa hii. Anaweza kusamehewa, bali sio kuhesabiwa haki.

79 Amepewa mwili wake, dhamana takatifu kutoka kwa Mungu. Hakuna mbwa jike, hakuna ndege, hakuna mnyama mwingine, hakuna kiumbe kingine kilicho jinsi hiyo. La. Ni yeye pekee. Kwa jambo hilo, yeye ni . . . Sababu ya dhamana hiyo kuwa takatifu sana, ni kwamba yeye anapaswa kuleta uhai duniani. Mwili wake ni tuta la kuoteshea uhai, hiyo ndiyo sababu amepewa dhamana hii takatifu.

80 Sasa hapa ndipo ambapo huenda msikubali, wengi, ninyi wanatheolojia. Hicho ndicho kilichoitia unajasi jamii yote ya binadamu, ni ule uzinzi hapo mwanzoni. Tuta lake la uzazi lilichafuliwa. Akazaa wale mapacha, Kaini na Habili. Tendo moja, watoto wawili. Yachunguzeni Maandiko. A-ha.

81 Angalieni sasa. Tunaona ya kwamba mwili wake ni tuta la kupanda mbegu, na kwa hiyo ni dhamana takatifu, asiuchafue huo. Sasa, ninazungumza sasa, nikileta jambo hili kwenye kielelezo, kuwaonyesha mahali ambapo Kanisa linasimama. Sizungumzi juu yenu ninyi wanawake. Chochote mlicho, hiyo ni kati yenu na Mungu, ama ninyi wanaume. Bali ninazungumza juu ya Kanisa na Kristo.

82 Sasa, hii amepewa, apate kuleta uhai ambao ni Mungu pekee anayeweza kuutoa. Mumewe anaweza kuwa ndiye mbebaji wa

mbegu zazi, bali inabidi Mungu atoe huo uhai. Hiyo ni kweli. Hauna budi kuja. Uhai wote hauna budi utoke kwa Mungu. Uhai wowote unapaswa utoke kwa Mungu. Ukiisha kupotoshwa, basi hicho ndicho kinacholifanya jambo hilo kuwa dhambi, lakini uhai hauna budi utoke kwa Mungu. Yeye ndiye mwanzilishi wa uzima. Sasa yeye ana ninii takati-. . . mmoja . . .

83 Ninataka kutaja mambo matatu hapa ambayo hapaswi kuyaacha. Sasa, ninaponena, shikilieni kanisa mawazoni mwenu wakati ninapoliongea jambo hili kwa mwanamke wa kawaida, kama vile Paulo anavyofanya hapa, katika mlango wa 7 wa Warumi.

84 Yeye ana dhamana takatifu ya uadilifu aliyokabidhiwa na Bwana wake, uadilifu fulani. Hakuna kitu kingine kilicho nao ila mwanamke. Vema. Amekabidhiwa huo na Mungu. Hapaswi kuchafua uadilifu huo.

85 Akithubutu kufanya jambo fulani baya, hana budi kulitubia kwa mumewe kabla hajamkubali, na aliweke hilo sawa. Vivyo hivyo na kanisa lililoolewa na torati, halina budi pia kuja mbele za Kristo, kabla ya ndoa ya pili. Hana budi kutubia hilo. Asipolitubia, na aishi na mumewe kwa miaka kumi na kisha alitubie, mumewe ana haki ya kumtaliki na kuoa mwanamke mwingine. Hayo ni Maandiko. Uasherati ni maisha machafu.

86 "Yusufu, usihofu, kumchukua Mariamu mkeo, kwa kuwa mimba yake ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu." Alikuwa ameazimu kumwacha kwa siri, mnaona, baada ya yeye kuwa amekwisha kumchumbia. Unapomposa msichana, kulingana na Mungu, umekwisha kumwoa.

87 Angalia sasa. Yeye ana dhamana takatifu ya uadilifu ambayo amepewa, aliyokabidhiwa na Bwana. Mungu alimpa uadilifu huo. Kama tu ilivyokuwa katika bustani ya Edeni, yeye anaweza kusema "ndio" ama "la." Yeye ana dhamana takatifu ya utu uke aliokabidhiwa, ambao hapaswi kuuharibu. Utu uke ninaonena habari zake hapa ni mwenendo wake, tabia yake mbele za wanaume. Si kumruhusu kila mwanamume . . .

88 Huangalia kwenye skrini hizi kuwaona hawa wachezaji maarufu wa sinema wakibusiana, na kukumbatiana, na kupapasana, na kukaribia, juu ya hawa wanawake. Mwanamke anayefanya jambo hilo, ni mwenye tabia mbaya. Huenda akawa ni mwadilifu, hata hivyo. Lakini, unaona, moyoni mwake . . . Wakati, hizo tezi, tezi za jinsia, zimo mdomoni. Mwanamume akimbusu mwanamke, kwa kweli, kwa uwezekano, amefanya uzinzi. Tezi za jinsia ziko kwenye mdomo wa mwanamke na kwenye mdomo wa mwanamume. Angeweza kumbusu mkononi, isingechanganyikana kupitia tezi zao za jinsia. Bali tezi za jinsia ziko midomoni. Na mnaona upuuzi huu wote huko—huko Hollywood siku hizi, huku kupapasana kote na kufanya mapenzi na wanawake, na kadhalika, na wasichana wadogo wakiangalia

hayo yote. Si ajabu uadilifu wetu umeoza na kuharibika, na ni mchafu, unaona, kwa sababu hayo yanaanikwa mbele ya watoto. Hiyo ni kweli. Haina budi kuwa hivyo kwa ajili ya siku ya mwisho.

89 Sasa wekeni kanisa mawazoni. Linabusiana na kupapasana, na kujichanganyisha na kila kitu ila Neno, linamruhusu Ibilisi, na elimu na utafiti wa kisayansi, na kadhalika.

90 Wakati, mambo ya sayansi, elimu, kila kitu, ni kinyume kabisa na Mungu. Mfumo wote wa ustaarabu tulio nao siku hizi ni upingakristo kabisa. Mfumo wa elimu ni upingakristo. Ustaarabu ni upingakristo. Unampinga Mungu. Unasema, "Ati dhidi ya ustaarabu?" Mungu atakuwa na ustaarabu, moja ya siku hizi, ambao hautahusishwa vyovyote na mauti. Ustaarabu huu wa kisasa umeletwa na Shetani. Nitawathibitishieni jambo hilo, Bwana akipenda, usiku wa leo, kutoka katika Biblia. Mambo yote haya ni ya Shetani. Ustaarabu wetu mpya hautakuwa na lolote la vitu hivi ndani yake.

Mwanamke ana huu utu uke mtakatifu.

91 Si ajabu kwamba wanaume wanatenda mbele ya wanawake jinsi wanavyotenda, ni kwa sababu wanawake wanajianika mbele ya wanaume jinsi wanavyofanya. Yeye anajitokeza hapa nje na kaptura, na nguo za kubana, na nguo za wanamume na kadhalika, huko mitaani, akikatika-katika. Hata aseme nini, anaweza awe msafi sana kwa mumewe awezavyo kuwa, lakini, machoni pa Mungu, "Yeye ni mzinzi." "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Naye alijianika awe hivyo.

Na hivyo ndivyo kanisa limefanya hasa na ulimwengu.

92 Angalia. Amekabidhiwa huo: uadilifu mtakatifu, utu uke mtakatifu, halafu na umama mtakatifu, kumheshimu mumewe.

93 Hebu angalia tu siku hizi. Katika miji fulani, miji mingi, hata wana karamu kubwa katika kile wanachoita jumuiya, wafuasi wa kanisa, pia. Wanaweka kofia zao sakafuni, kisha wote wanalewa pombe na kutupa funguo zao humo ndani. Kila mwanamke anaenda na kuchukua ufunguo kutoka kwenye kofia fulani, ya mwanamume atakayeishi naye kwa wikiendi hiyo. Kila aina ya karamu za aina hiyo! Mambo ambayo, nina mengi sana ya kusema hapa, Bwana akipenda, sina wakati wa kuingilia jambo hilo. Uchafu kama huo!

94 Na kanisa ni baya namna hiyo hiyo, kweli, linafanya uzinzi na kila kitu, wala halina shughuli ya kuingilia mambo hayo. Linapaswa kudumu na Neno.

95 Majengo ni sawa. Hospitali ni sawa. Mambo haya mengine yote ni sawa. Mipango ya elimu, hiyo ni sawa. Hatuna budi kuishi hapa, hatuna budi kusoma, kuandika. Hiyo ni mojawapo ya mambo ya mfumo wa maisha.

96 Kama vile ambavyo, hatukupaswa kuvaa nguo zozote, hapo mwanzo. Nitahubiri juu ya jambo hilo, baadaye juma hili, Bwana akipenda. Lakini inatubidi kuvaa nguo kwa sababu Mungu alitupa nguo. Lakini, hapo mwanzo, hatukuzihitaji. Tulikuwa tumetiwa utaji.

97 Sasa mwanamke ametiwa utaji wa dhambi yake. Hata hajui kwamba anatenda dhambi, mnaona, kama alivyokuwa wakati ule. Kwa ninii . . . Sasa yeye ametiwa utaji na Ibilisi; kule nyuma alikuwa ametiwa utaji na Mungu. Ndiyo tofauti yake.

98 Sasa tunaona ya kwamba yeye amepewa dhamana hii takatifu ambayo hapaswi kuiharibu: ya utu uke, atende, adumishe tabia yake, awalee watoto wake, awe na heshima kwa mumewe.

99 Siku hizi, hawajishughulishi na jambo hilo kabisa. Yafaa mketi ofisini kwangu wakati mwingine mwone wanaume wakiwaleta wake zao, ambapo wanajaribu kuweka sawa mambo yao kwa Mungu na kutubia kuhusu wanaume wote walioishi nao, na chochote kile, tangu walipoolewa. Loo, unasema, "Hao ni . . ." La. Hao ni Wapentekoste. A-ha. Hao wengine hawatakuja. Kwa hiyo ni . . .

100 Ninazungumzia jinsi jambo hilo linavyoweza kupotea, unapoanza kujichanganya na ulimwengu, kanisa, na mitindo yote na mambo kadhaa tuliyo nayo. Hatuko tena kama Pentekoste ya asili ilivyokuwa zaidi ya vile mchana ulivyo mbali na usiku. Tumechepuka mahali fulani, tukaingia katika machafuko fulani ya giza mahali fulani, na tukapotea.

101 Ni dhamana takatifu jinsi gani! Ni jukumu la namna gani kwa mwanamke! Sasa angalia ni kwa nini yeye ni mfano wa Kanisa, ambalo lina wajibu ule ule. Kama vile mwanamke alivyo na wajibu mtakatifu kwa umama wake, kwa uadilifu wake, kwa mume wake, Kanisa lina wajibu mtakatifu kwa maombi na kwa Neno, na kwa Kristo, kama vile tu mwanamke alivyo nao.

102 Na kama vile mwanamke anavyochukuliwa kwa urahisi na mwanamume mwingine; hali kadhalika kanisa linapoenda kando kwenye mipango hii ya kimadhehebu, na miradi ya ujenzi na shule, na kadhalika. Sina kitu dhidi ya hiyo. Hiyo yote ni sawa. Yanakidhi matakwa yao. Bali haininii . . .

103 Yesu kamwe hakusema, "Enendeni, mkajenge shule." Alisema, "Mkahubiri Neno."

104 Hapo ndipo wanapolipuuza. Si kuunda mashirika, hospitali na kadhalika. Hayo ni sawa, bali huo sio wajibu wa Kanisa. Wajibu wao ni kuhubiri Injili, bali tumefanya kila kitu isipokuwa hicho. Nasi tumechukuliwa na mkondo, kama tu Shetani alivyofanya, na kulichanganya na Injili fulani, kitu kingine, na kitu fulani kingine, mpaka linakuwa ni bonge la upuuzi. Upotovu, hata ninii yetu yote, dunia nzima! Angalia mwelekeo wa dunia.

105 Nilikuwa nikisoma *Readers Digest*, hapa si muda mrefu uliopita, ambapo wasichana wadogo wanafikia ukomohedhi wao, na wanaume, badiliko la maisha, kati ya umri wa miaka ishirini na ishirini na mitano. Wanapitia katika umri wao wa makamu. Upotovu, (kwa nini?) kwa sababu ya utafiti wa sayansi wa vyakula na kadhalika ambavyo vimeharibika, tukatoka kwenye vitu vya asili tunavyopaswa kuweka mwilini mwetu. Sisi si kitu ila ni lundo la uharibifu unaokufa.

106 Sasa, hivyo ndivyo kanisa lilivyo, pia. Liko katika hali hiyo hiyo.

107 Lenyewe ni mfano. Lina uadilifu ule ule wa thamani kwa Roho, liliopewa, kudumisha Roho na Neno, wala kamwe lisizini na kitu chochote cha ulimwengu wala chochote kile. Lidumu bikira kwa Neno, kama vile mwanamke anavyopaswa kudumu mwadilifu kwa mumewe. Ni dhamana takatifu, kuliheshimu Neno la Bwana Wake zaidi ya kila kanuni ya imani ya kujibunia, hekima, madhehebu yoyote yaliyopo. Kanisa limepewa dhamana hiyo.

108 Wakisema, "Vema, kanisa langu..." Sijali kanisa lako linaamini nini. Kama linahitilafiana na Neno la Mungu, achana nalo.

109 Biblia ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, milele." Marko 16 ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kanisa likihubiri tofauti na Hilo, usithubutu. Wewe lifie jambo hilo. Zaliwa mara ya pili, katika Neno la Mungu. "Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe." Huo ndio umbali lililotakiwa liende. "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, ulimwenguni kote, na kila kiumbe kitakachoamini." Unaona jinsi ambavyo tumeiacha? Hakika. Bali Kanisa linawajibika Kwake.

110 Lakini sasa angalia jinsi ambavyo, Hollywood, imeondoa mambo ya uadilifu kutoka kwa wanawake wetu.

111 Nimeketi hapa nikimwangalia maskini mwanamke mzee mpendwa, Dada Schrader, wengi wa hao wanawake hapa, na kule nyuma, na Dada Moore hapa, hao mama wa zamani wanaokumbuka miaka michache iliyopita. Kama mama zao, ama hata wao, wangalitoka watembee huko nje mitaani, jinsi ambavyo baadhi ya wanawake hawa wanavyotembea siku hizi, wafuasi wa kanisa, wangalimfunga mwanamke huyo kwa kuwa mwenda wazimu. "Alisahau kuvaa sketi yake." Vema, kama ilikuwa ni wenda wazimu wakati huo, ni wenda wazimu sasa.

112 Vema, angalia, dunia nzima inathibitisha kwamba imeingia kichaa. Angalia mauaji na mambo yanayoendelea sasa ulimwenguni. Unaona? Wazimu!

113 Kitu hicho chote kinakuja kutimiza Ufunuo. Huenda tukalifikia, juma hili. Ambapo, vitu hivyo vya kutisha sana, hivyo si vya maumbile ya kawaida. Hivyo ni vitu vya

kiroho, ambavyo vinawafanya watu kuipigia miamba na milima mayowe, na chochote kile, viwaangukie.

114 Ule wazimu mtupu, ambao ulimwengu huu utaingiwa nao, mara moja, takriban upo sasa hivi. Mbona, unaona nyayo zake. Huo hapo. U—unatembea moja kwa moja huko mtaani, moja kwa moja kwenye mabenchi ya kanisa, wazimu mtupu, kufanya mambo ambayo mwanadamu asingefikiria kuyafanya huku akiwa amestaarabika.

115 Angalia kile Hollywood imetenda kwa mwanamke. Angalia jinsi mambo yalivyo. Imepora maadili matakatifu ya mwanamke. Tungeweza kuendelea na kuendelea. Unaona?

116 Yote haya alipoteza. Aliyapotezaje? Kwa sababu kulikuwako na chombo kijanja kinachoitwa kanisa, kama vile ilivyokuwa katika bustani ya Edeni. Mtu mjanja, Ibilisi, aliingia kanisani kama tu vile alivyofanya katika bustani ya Edeni, na kumdanganya aingie kwenye jambo hilo. Amedanganyika. Mwanamke anawazia; hamaanishi kutenda mabaya.

117 Hawa hakutaka kufanya makosa. Haikuwa ni makusudi. Lakini yeye . . . Biblia ilisema, katika Timotheo wa Pili, Timotheo wa Kwanza 3, "Alidanganywa." Na *kudanganywa* si wakati unapotenda jambo makusudi. Ni wakati unapodanganywa ukaingia kwenye kutenda jambo hilo.

118 Na hivyo hasa ndivyo ilivyotukia leo. Yeye amedanganywa, na televisheni, na magazeti, na watu hawa, hawa, mambo haya yote mazuri ya wanayoyaendea, huko nje mtaani. Wasichana wa kisasa, wanaangalia magazeti na wanaangalia sinema. Wanaangalia mtaani. Wanaona nguo madukani. Jinsi Shetani, kile chombo kikuu cha—cha jahanamu, alivyoshuka miongoni mwa watu na kuwadanganya wakazama katika mambo haya! Na mwanamke anafikiri kwamba yeye yuko salama. Naye amekufa na wala hajui. Yeye yuko mbali na Mungu. Mnaona jinsi alvyyopoteza haya yote, na jinsi chombo hicho kilivyokuwa cherevu?

119 Leo, ninawatakeni mwone. Yesu alinena habari zake. Pia, kama ungetaka kusoma jambo hilo, Yesu alitamka ya kwamba jambo hili lingetimia (Je! ulijua jambo hilo?) katika saa Zake za mwisho, kabla tu ya kusulubiwa Kwake. Hebu tu na tulisome, Luka Mtakatifu, m—mlango wa 23, na kwa muda mfupi tu, kama somo la Shule ya Jumapili. Tuanzie kwenye kifungu cha 27, ninaamini nimeliandika hapa. Yesu akielekea Kalvari. Sikilizeni ninapolisoma. Vema. Luka Mtakatifu 23:27, ninaamini, ndipo tunapolipata. Muhtasari wangu umeliandika hivyo. Naam. Hili hapa.

> *Mkutano mkubwa wa watu wakamfuata, na wanawake waliokuwa wakijipiga vifua na kumwombolezea.*

*Yesu akawageukia, akasema, Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi, bali jilílieni nafsi zenu, na watoto wenu.*

*Kwa maana tazama,* siku—*siku zitakuja,... watakaposema, Heri walio tasa, na* tumbo *lisilozaa, na maziwa yasiyonyonyesha.*

120 Wazieni, siku hizi, ni aibu kwake kuzaa mtoto. Mnaona?

*Ndipo watakapoanza kuiambia milima, Tuangukieni; na* ki-...*na vilima, Tufunikeni.*

*Kwa kuwa kama wakitenda mambo haya katika mti mbichi, watafanyaje katika mkavu?*

121 Akinena juu ya siku ambapo wanawake wasingetaka watoto tena. Wanataka mbwa ama paka, ama kitu kama hicho, bali hataki watoto tena. Kwa nini? "Eti yeye ni maskini Bibi Kizee kama ana mtoto." Mnaona? Yeye hataki. Hayo ni—hayo ni matamshi ya Hollywood. Haitaki mwanamke wake awe maskini Bibi Kizee. Kwa hiyo mwanamke ataninii, mume atafanyiwa upasuaji ama mke atafanyiwa, mmoja wao, ambao utawazuia kupata watoto. Kamwe hawataki watoto.

122 Yesu alinena juu ya jambo hilo. Naye alisema nini? "Wakati huo wataanza kuililia miamba na milima 'ituangukie.'"

123 Mwanamke atapanga uzazi, kusudi aweze kwenda kwenye karamu. Hawezi kusumbuliwa na jambo la kunyonywa na mtoto. "Mtoto atamharibia umbo. Akiwa mja mzito, itakuwa kwamba, itamuumbua umbo. Hataonekana kama alivyokuwa akionekana." Naye mumewe, ni mjinga vya kutosha kumwacha aendelee hivyo. Hatamzalia mtoto.

124 Yesu alinena juu ya jambo hilo. Naye alisema, ya kwamba, "Walipokuwa wakifanya jambo hili, wakati huo ndipo wataanza kuililia miamba iwaangukie." Ni Kuja kwa Bwana.

125 Wanalipa fedha nyingi kununua paka, mbwa, wapate kuwalea. Hiyo ni kweli. Hana budi kulea kitu fulani, kwa kuwa ni asili aliyopewa na Mungu.

126 Ninaona. Mimi huwinda wanyama wakubwa. Dubu mzee mwishoni mwa mwaka, wakati amekwisha kutana na dubu dume, yeye huwa na watoto wakati huo waliozaliwa. Wao ni watoto wakubwa vya kutosha, labda wana uzito wa ratili mia moja ama zaidi. Atawafanya waambae na kubumbwaa peke yao, kwa sababu yeye yuaenda kuzaa vitoto vingine zaidi. Wanazaliwa Februari. Dubu hajui lolote kuhusu jambo hilo.

127 Wanazaliwa katika vifuko vidogo. Inashangaza jinsi Mungu anavyowafanya wafungue vifuko hivi vidogo, wao wenyewe, vidogo...kama vifuko vidogo vya selofeni. Wanajitegemea. Mama yao amelala fofofo. Hajala chochote tangu Oktoba, na hii ni Februari. Vinakuja na kumnyonya mpaka katikati ya Mei.

128 Ndipo wakati anapoviona vitoto vyake, ni vitoto vikubwa vizuri, labda vina uzito wa ratili kumi na tano hivi, kumi ama kumi na tano kila kimoja. Vimemnyonya. Jinsi anavyopata maziwa, hilo ni la Mungu. Yeye anaishi, yeye mwenyewe, na kutoa maziwa kwa ajili ya vitoto vyake.

129 Ndipo basi endapo hakuzaa, wala hana watoto wowote, atawatafuta hao wa mwaka huo, watoto wa mwaka jana, na kuwalea kwenye msimu wote wa kiangazi, kwa maana ni silika aliyopewa na Mungu. Hana budi kulea kitu fulani.

130 Na kama mwanamke hatamzalia mumewe mtoto, yeye atamchukua mbwa ama paka, ama kitu fulani. Hana budi kulea kitu fulani. Ni maumbile fulani. Lakini kumzalia mumewe mtoto, na kumlea akamtumikie Mungu, hilo liko mbali sana naye. Anapaswa. Loo, yeye angeninii. . .Loo, angefedheheshwa sana, kama angalifanya hivyo, mbele ya jumuiya yake inayopenda dhambi za wanawake sampuli ya mwaka huu wa 1965.

131 Ni picha ya kweli ya kanisa la kisasa siku hizi! Wala kanisa la kisasa halitaki yeyote ya watoto hawa hapa wa Matendo 2:38, wanaopiga makelele, wanaopaza sauti, wanaonena kwa lugha, wamkaribie. Naam. Naam. Unaona? Naam. Hataki yeyote wao anayeshangilia, na kulia, na kupiga kelele, "Amina! Haleluya!" Mbona, mtoto kama huyo angemwondoa mara moja kutoka kwenye dhehebu lake. Wangelikuwa na mmoja kama huyo katika moja ya makanisa hayo, mbona, wangemtupa nje upesi sana.

"Mbona mnaachilia upuuzi kama huu uendelee?"

132 Kwa hiyo, unaona, yeye ametiwa mimba na kitu fulani, maana anapata wafuasi kila wakati. Bali hataki yeyote wa hao anaowadhania kwamba ni watu duni wa Matendo 2:38 wanaopiga makelele, kupiga mayowe, na kupayukapayuka. Bila shaka huyo angemwaibisha. Angemwathiri pamoja na jumuiya yake ya kanisa lenye elimu, la kimaadili na la kisayansi ambalo yeye alikuwa ni mfuasi wake hapa. Wangemtupa nje, kwenye kikao kingine cha baraza. Haliwezi kuzaa. Kwa hiyo halitaki kutiwa mimba na Neno, kwa kuwa Neno linaweza tu kuzaa wa aina hiyo.

133 Likiwa limezaliwa kwa Roho wa Mungu, lina Roho wa Mungu ndani yake. Hakuna kujiunga na kanisa kiakili wala kuendea kanuni ya imani, nywele zilizokatwa, uso uliopakwa rangi; hakuna kitu kama hicho kote ndani Yake. Hupati jambo hilo katika Neno la Mungu. Unapata mtoto wa mtindo wa kale, aliyetakaswa, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, aliyezaliwa na Roho wa Mungu, akipiga makelele, akipiga mayowe, akipaza sauti, akimsifu Mungu.

134 Hayo kwa jumla yako mbali naye. Hataki mambo Hayo. Loo, la, bwana! La, hasha. Anafanya nini basi? Kwa hiyo anazaa mapacha ya jamii ya Yezebeli, wenye uso uliopodolewa,

wanaovaa kaptura, "vipaka" haramu, ndivyo wanavyowaita, nafikiri ndivyo. Mnaona? Nafikiri wanawaita vipaka. Mnaona? "Angalia yule paka anayeenda kule," wanasema, ama kitu kama hicho, unajua.

135 Alizaliwa, ama kuolewa, akaunganishwa na mume wake wa kwanza, Adamu wa kwanza, kwa mke mzinzi wa Hawa, mke wa kwanza wa Adamu. Unasema, "Ati mzinzi?" Hakika alikuwa mzinzi. Lakini, loo, anadai ya kwamba Adamu huyu, Adamu huyu wa kwanza, amekufa. "Loo, hakika, alikufa zamani za kale. Nimezaliwa mara ya pili, tena," akasema, "na bila shaka nimeolewa na Adamu wa Pili, Kristo, lile Neno."

136 Jinsi gani? Angalia kile anachopenda. Angalia mpenzi wake, unataka kuona anapendana na nani. Neno linasema *Hivi*, bali yeye alisema, "Kanisa langu linasema *hivi*." Basi yeye anapendana na nani? Mume wake ni nani? Matunda yake mwenyewe yanathibitisha kwamba yeye ni nani. Kweli kabisa, yanaonyesha kwamba yeye ni nani. Angalia. Alizaliwa, kwanza, kwa Adamu, kwa maana huko ndiko kuzaliwa kwake kwa kimaumbile. Unaona? Wala kamwe hakuacha hilo. Huyo ni mpenda dunia. Anadai ya kwamba amezaliwa mara ya pili, kwa Kristo. Lakini mpenzi wake, angalia, ni Adamu, bado, kwa sababu anaipenda dunia.

137 Na jambo lingine—lingine, angalia anazaa watoto wa aina gani. Hilo linaonyesha baba yao ni nani, kwamba ni Adamu wa kwanza ama Adamu wa Pili. Kanisa likimzaa mtoto wa Adamu wa Pili, anatenda kama Adamu wa Pili anavyotenda, kama walivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Hao ndio watoto wa kweli wa Adamu wa Pili. Mnaona? Sawa. Tabia yao ni kama ya baba yao na mama yao. Naam, bwana. Binti zake, wamejipodoa uso, wamekata nywele, wanavaa nguo za wanaume, suruali ndefu. Biblia ilimwambia "asifanye hivyo." Anakata nywele zake. "Ni aibu kwake."

Unasema, "Funga mdomo, juu ya jambo hilo."

138 Hivyo ndivyo Neno linavyosema. Ninaonyesha tu maumbile. Hivyo ndivyo anavyofanya.

139 Wanawe, wanawe waliozaliwa naye, wanategemea elimu, kisomo, shule fulani ya Biblia, wanavyoziita, chuo fulani kikuu ambacho kinadhaniwa ni cha zamani sana, kikiwaangua, katika namna fulani ya mtindo wa kiangulio. Wenye kupenda madhehebu, wa kidini kama Kaini, wanaharamu tu kwa Neno kama Kaini alivyokuwa; naam, waovu tu kama yeye, wanaharamu tu kama Kaini alivyokuwa, hakika, wenye kupenda madhehebu. Mnaona ni kitu gani?

140 Mungu hajawahi kamwe kuunda madhehebu. Daima amekuwa dhidi yake. Neno Lake linayapinga.

141 Lakini wao wanashikilia jambo hilo kabisa, kwa hiyo unaona kile wanachozaa. Hilo linaonyesha baba yao na mama

yao ni nani. Kweli kabisa. Kweli. Ni wanaharamu tu kama Kaini alivyokuwa. Alizaa mtoto wa aina hiyo kutoka kwa Hawa. Waliondoka kwenye Neno, halafu angalia kile alicholeta. Hicho ndicho kanisa lilicholeta hasa, kitu kile kile.

142 Ninaweza kuwathibitishia, kwa Neno, ya kwamba hapo ndipo elimu na ustaarabu vilikotoka, kupitia kwa Kaini. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa kuwa wanadai . . . Lakini wao—wao wanadai kuwa ni wana wa Mungu, lakini wamezaliwa kimadhehebu, wamefunzwa kwenye shule ya kimadhehebu, chochote kile. Hiyo ni kweli kabisa. Wajanja, werevu! Jamani! Ndivyo alivyokuwa yule nyoka, baba yao. Kweli. Ni wahubiri wajanja kabisa na wa kisayansi kama Kaini alivyokuwa. Unaona? Ni jambo lile lile kabisa.

Unasema, "Ndugu Branham, hiyo ni kweli?"

143 Fungua Mwanzo 4:16 na uangalie. Rudi nyuma hapa katika Mwanzo 4:16, kwa dakika moja tu, utaona jinsi ilivyotukia.

> *Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana, akakaa katika nchi ya Nodi, mashariki mwa Edeni.*
>
> *Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji, akauita Henoko, kwa jina la mwanawe.*

144 Na kuendelea mpaka kwa Tubali, na kuendelea, kwa kuwa walianza, wakaja wabuni vyombo, muziki, na kadhalika. Ustaarabu ulitokana na Kaini, kweli, kujenga miji, vyombo vya muziki. Wanasayansi walitokana na Kaini, ule uzao wa nyoka. Sasa angalia kifungu cha 25.

> *Adamu akamjua mke wake tena;*

145 Sasa, yeye alimjua mara moja naye akazaa watoto wawili. Yachunguze Maandiko. Alimzaa Kaini na Habili. Tendo moja, na watoto wawili. Unasema . . .

146 Waliniambia, si muda mrefu uliopita, isingewezekana, kutukia. Tuna kesi kule Hollywood. Ati Hollywood? Tuna kesi huko Tucson sasa hivi, inayoendelea mahakamani. Mwanamke fulani alizaa mtoto mweusi na mtoto wa kizungu, kwa wakati mmoja. Wanasema mwanamke hawezi kufanya hivyo. Anaweza kuwa na mayai mawili rutubifu, pia. Wana kisa hicho hivi sasa mahakamani. Najua mbwa watafanya hivyo. Wanyama watafanya hivyo. Na mwanamke huyo anao kule, huyo mwanamume wa kizungu akasema, "Nitamlea mtoto wangu mwenyewe, lakini si huyo mwingine."

147 Ndipo mwanamke huyo akakiri. Aliishi na mumewe asubuhi hiyo, na huyo mtu mweusi alasiri hiyo. "Kama ni katika," daktari anasema, "muda wa saa ishirini na nne, jambo hilo litatukia endapo kuna yai lingine rutubifu pale." Na hapo huyo mama alifanya hivyo.

148 Na hivyo ndivyo hasa ilivyotendeka hapa. Kaini ambaye... Shetani, asubuhi hiyo, katika yule nyoka; na Adamu, alasiri hiyo. Wakati aliponinii... Naye akajifungua wototo wawili.

> *Sasa Adamu akamjua mke wake tena,* (mara ya pili); *akazaa mwana mwanamume...*

149 Kumbukeni, hakuna mahali popote katika Biblia ambapo palisema Kaini alikuwa mwana wa Adamu. Ilisema, "Alikuwa wa yule mwovu," si Adamu, "Ibilisi."

> ...*akamjua nanii wake* (mara ya pili), na akamjua... ndipo *akazaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi; maana alisema, Mungu ameniwekea*...(Huyo hakuwa Uzao halisi.)...*ameniwekea uzao mwingine mahali pa* Adamu*; kwa sababu Kaini alimwua.* Kwa hiyo...
>
> *Sethi naye akazaa mwana; akamwita jina lake Enoshi. Hapo ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la* B*WANA.*

150 Si kutokana na wa Kaini, kizazi cha ukoo huo, bali kutokana na ukoo wa Sethi.

Kwa hiyo, "Kaini ndiye yule mwovu." Hapo ndipo yule nyoka anapokuja.

151 Sasa angalia. Biblia inasema waziwazi hapa, ya kwamba, "Mume wake wa kwanza hana budi awe amekufa," si kutalikiwa tu. Hana budi awe amekufa.

152 Ndiyo kwanza nimekwisha kuhubiri juu ya *Ndoa na Talaka*, nanyi nyote mnajua kuhusu hilo. Mimi sizungumzii sasa, kwa jumla, kusanyiko hili hapa, bali kote nchini. Vema. Sasa mnaona lililotukia pale, katika *Ndoa na Talaka*. Wakati hilo...?... Mihuri Saba ilifunguliwa, ambayo ilileta Ukweli halisi wa jambo hilo.

153 Kwa hiyo, kuolewa na Adamu wa Pili, Kristo, aliye Neno, huna budi kujitenga kwa kufa, kutoka kwa mume wako wa kwanza wa kimadhehebu, maana hakuna moja ya hayo linaloweza kuchukua Neno lote la Mungu. Hebu nionyeshe tu mahali lilipo hilo. "Loo," unasema, "langu." Jamaa huyo mwingine anasema na lake, pia. Yawekeni pamoja, nanyi mtaona nyote wawili mko makosani, mara mnapounda madhehebu. Someni Ufunuo 17. Kwa hiyo, unaona, huna budi kufia kitu hicho.

154 Sasa, sizungumzii kusanyiko hili la mahali hapa. Ninazungumzia kote nchini kwa jumla. Huna budi kufa kwa mume wako wa kwanza. Kama umeunganishwa na Kristo na ungali umeolewa na madhehebu, wewe ni mzinzi. Wewe ni Laodikia.

155 Kanisa kote nchini, tunamfuata Yesu Kristo, lile Neno. Ili upate kuwa katika Bibi-arusi, inakupasa kuolewa tena na Neno la Mungu, ambalo ni Kristo. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno,

Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu."

156 Ilimradi unashikilia mapokeo ya madhehebu ya mwanadamu, unaitwa, katika Neno la Mungu, "Mzinzi." Alimradi wewe ni mpenda kanuni za imani za kimadhehebu, ukiwa ni mfuasi wa kanisa la kimadhehebu ambalo linakana Neno, wewe ni "mzinzi," ndivyo Biblia ilivyosema.

157 Yesu alisema, "Huwezi kuitumikia miungu miwili kwa wakati mmoja. Aidha utamtumikia Mungu ama mamoni." *Mamoni* ni "ulimwengu." "Yeye aipendae dunia, au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake." Uzao wa Mungu hauwezi kuwa ndani yake wakati uo huo (kumpenda Mungu) kuipenda dunia kumo ndani. Wakati Uzao wa Mungu unapotenda kazi kupitia kwako, hilo ni Neno la Mungu. Kuipenda dunia hakuwezi kuwamo mle ndani wakati uo huo. Sasa ziko wapi nywele fupi, na zile kaptura, na nyuso zilizopodolewa? Sasa ziko wapi?

158 Huwezi kuwa mwadilifu kwa Kristo, Neno la Mungu, na uyatumikie madhehebu yaliyoundwa na mwanadamu wakati uo huo. Ni kinyume cha Neno. Paulo alisema hapa. "Ni wapi?" Warumi 7.

159 Wala huwezi kumzalia Mungu wana, wa Neno Lake, kwa kundi hili haramu la kimadhehebu. Huwezi kufanya hivyo. Katika kiatamia chako, huwezi kumzaa mwana wa Neno la Mungu. Ninazungumza na kanisa. Lakini hata hivyo unadai kuwa wewe u wa kidini sana. Kaini alikuwa vivyo hivyo, yule mwana wa ukahaba wa Hawa, wa kidini sana, alijenga madhabahu na akatoa sadaka, na akalipa zaka zake na kufanya kila kitu ambacho mtu mwingine yeyote wa kidini angefanya. Bali alishindwa kutimiza hilo Neno. Alishindwa kupata ufunuo.

160 Na ufunuo ndicho kitu cha pekee, ufunuo wa Neno. Ni nini. . .Ufunuo ni nini? Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda." Imani ni ufunuo: kwa maana Imani imefunuliwa kwako.

161 "Habili, kwa Imani, alitoa kwa ufunuo (Imani), alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi kuliko ile ya Kaini."

162 Kaini alifikiri walikula matofaa. Wangali wana wazo hilo, bali haikuwa hivyo. Ilikuwa ni uzinzi, uzao wa nyoka. Na pale wakati Mihuri Saba ilipofunguliwa, ililifunua jambo hilo na kulithibitisha. Kitabu changu ndiyo kwanza kitoke juu ya jambo hilo. Wazia, tuna elfu moja hapa sasa. Unaona? Angalia. Hilo ni la Kimaandiko, kutoka Mwanzo mpaka Ufunuo.

163 Wakati wa mwisho, miti yote miwili inafikia kwenye kuzaa mbegu na kujithibitisha yenyewe. Sisi hapa tumewasili, leo hii, Laodikia na Bibi-arusi, liko wazi tu na ni zuri sana kama liwezavyo kuwa katika Maandiko, na pia liko moja kwa

moja mbele ya nyuso zenu. "Huwezi kumtumikia Mungu na mamoni." Huwezi kuwa Mkristo mwadilifu anayeamini Biblia na ujihusishe katika mambo ya kimadhehebu. Huwezi kufanya hivyo kamwe wakati uo huo. Mmoja sharti awe amekufa, na kumwacha huyo mwingine aishi.

164 Wala huwezi kumzaa mwana wa Neno la Mungu. Wala kanisa haliwezi kuzaa. Hawataki mmoja wa hao watoto, wanaopiga mayowe, wanaopiga makelele na kunena kwa lugha, na mambo hayo yote. Wao, huwezi kufanya jambo hilo katika kanisa la kimadhehebu. Hawatakupokea. Hawawazai namna hiyo. Wanawachukua na kuwapa mikono na kusema, "Kama unaamini, umempata. Ilimradi umeandikisha jina lako kwenye kitabu, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya." Unaona? Ni—ni watoto haramu kwa Neno, wangali wanadai kwamba ni wa kidini.

165 Kanisa limejazwa sana na hekima na maarifa ya Shetani, kanisa limekuwa hivyo! Wanawapeleka watu wao huko shuleni, kujifunza jinsi ya kusema "amina" ipasavyo. Wanawafunza jinsi ya kusema haya yote, na kuwa werevu sana. Ni kitu gani? Ni kutiwa mimba na Ibilisi. Shetani alimtia mimba Hawa kwa kitu gani? Kutokuamini Neno, kuleta watu wenye akili nyingi, watu wenye bongo, ndipo akayaharibu maumbile yote. Hivyo ndivyo limefanya hasa katika Neno siku hizi, kanisa. Limejitia mimba kwa shule za Biblia na vyuo, na vitu kama hivyo, kusoma, kuandika, hesabu, nao hawajui zaidi juu ya Mungu kuliko Mhotentoti anavyojua juu ya hekaya za Kimisri. Wanajua kanuni zao zote za imani, vitabu vyao vya sala, chochote kile, bali hawajui chochote kumhusu Mungu.

166 Wanajua wakati Neno limethibitishwa, wakati Mungu aliponena kule nyuma na kugawa Neno Lake kwa kila kizazi wakati vilipokuwa vinakuja. Huyu hapa Nuhu anakuja, naye akakihubiri kizazi kile.

167 Sasa, vipi kama Musa angalikuja, akasema, "Hebu na tujenge safina"? Angekuwa amepitwa na wakati kabisa. Lakini alikuwa ni nabii. Alikuwa na ufunuo wa Mungu.

168 Mungu alithibitisha jambo hilo kuwa ni Kweli. Aliwaleta wale wana huko, aliwatoa Israeli, na akaonyesha ile Nguzo ya Moto mbele zao, na akamthibitisha nabii; na akasema vile hasa Yeye angefanya, Naye akafanya hivyo.

169 Wao walisema, "Hebu Mungu asinene. Hebu anene Musa, tusije tukafa."

170 Akasema, "Sitazungumza nao tena namna hiyo, bali nitawaondokeshea manabii, nao watanena."

171 Huyo hapo Isaya amesimama pale, akasema, "Bikira atachukua mimba." Mtu kama yeye katika siku ambapo. . . Bikira atachukuaje mimba? "Maana kwa ajili yetu Mtoto Mwanamume amezaliwa: Mtoto amezaliwa, tumepewa Mtoto

Mwanamume. Ataitwa Jina Lake: Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Juu ya kiti cha enzi cha Baba Yake, Daudi, Yeye atatawala. Ufalme Wake hautakuwa na mwisho." Itakuwaje? Yeye hakujua. Alisema tu vile Mungu alivyosema. Haliwaziki, kiakili. Limepita utafiti wowote wa sayansi. Ni Neno la Mungu.

172 Sasa tunawafundisha wanafunzi wetu wa seminari katika kila namna ya thiolojia ya Biblia na mambo kama hayo, thiolojia ya kujibunia, humo mna wafuasi wa kanisa lililo Laodikia hasa, kama vile Mungu alivyosema itakuwa. Loo, jamani! Ninapoangalia jambo hilo, na linanifanya nitetemeke. Wametiwa mimba na mawazo ya kiakili! Inabidi uwe umehitimu sekondari ya juu kabla hata hujaingia. Huna budi kuwa na . . . huna budi kusimama mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili kabla hujaweza kufanywa mhudumu.

173 Ungeweza kuwawazia akina Petro, Yakobo, na Yohana wakienda mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili? Je! unakumbuka wale mia na ishirini kule juu, wasingeweza hata kuandika jina lao wenyewe? Ati wasimame mbele ya mtaalamu wa magonjwa ya akili, aone kama wao . . . kama ninii yao yote . . . kama tu tendohisia lao lilikuwa liko sawa, na kadhalika? Walikuwa na tendohisia, bali halikuwa la wazo la kiakili wala utafiti wa kisayansi. Lilikuwa ni la kupitia kwenye Nguvu za Mungu. Wakati Hilo lilipowashukia, hawakujua la kufanya ila ni kutenda tu lile Roho Mtakatifu alilosema watende. Hawakujali msomi yeyote, kile kanisa lilichosema, na yale makuhani waliyosema, kile *huyu* alichosema, *yule* alichosema. Walienenda kwa Roho; watu jasiri.

174 Yohana wa Kwanza 2:15, Yeye alisema, "Ukiipenda dunia, ama mambo yaliyomo duniani, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Unaona? Kwa hiyo unawezaje kutiwa mimba na Neno la Mungu ambalo linauhukumu ulimwengu, linaihukumu Hollywood, linahukumu mitindo yake yote, linahukumu karamu hizi zote na utovu wa adabu, na upuuzi walio nao katika jina la dini? Linahukumu kitu hicho. Neno linawezaje kumtia mimba mtu: lawezaje kumtia mimba mwanamke anayekata nywele, aliyejipodoa uso, anayevaa kaptura?

175 Mhubiri anawezaje, anayetoka kwenda hapa kwenye seminari, na anaangalia Matendo 2:38 na kuona ya kwamba hakuna mtu katika Biblia aliyepata kubatizwa katika vyeo hivyo, na kisha bado aseme yeye ametiwa mimba na Neno la Mungu? Anakwambia uongo! Aliuza haki zake za mzaliwa wa kwanza. Amefanya uzinzi dhidi ya Kitu kile kile alichosema. Ametengwa, katika talaka.

Mungu atakuwa na Kanisa adilifu, kweli kabisa, Bibi-arusi.

176 Biblia ilisema, "Neno halimo ndani yenu." Kwa hiyo unawazaa watoto wa namna gani? Wana wa kimadhehebu

waliotiwa mimba. Hakujakuwa na kifo cha kukutenganisha wewe na mpenzi wako wa kwanza.

177 "Je! akina Jones watawazia nini kama nikianza kulia na kunena kwa lugha? Watawazia nini kama nikibatizwa tena?" Ni upuuzi wa jinsi gani! Je! umeolewa na akina Jones? Umeolewa na kanisa? Umeolewa na Kristo, lile Neno?

178 Sasa, hiyo ndiyo sababu lingali linamzalia watoto. Lina watoto wa aina gani? Haya hapa baadhi ya majina wanayoitwa siku hizi: vipaka, mabitoozi, madubwana, marike, mariketa. Vipaka, mabitoozi, hao ni wafuasi wa kanisa. Hakika. Wote ni wanawe, wana wa Kaini, ambao ni wana wa yule mnyama mjanja, werevu wawezavyo kuwa.

179 Sasa angalia kwa makini kwa muda mfupi, kwa macho yako mwenyewe ya kiroho, nafsi yako. Hebu angalia kila upande. Ninawazungumzia kote nchini sasa. Angalia tu kwa dakika chache, ninyi mlio huko nje kwenye Maskani ya Branham, ninyi mlio huko kwenye maskani za Pwani ya Magharibi, na Arizona, na kila mahali mlipo. Hebu jiangalieni kwa dakika chache. Unasema, "Ujumbe huo unaohubiri, Ndugu Branham, ni makosa." Hebu jiangalie mwenyewe kidogo. Hebu Roho Mtakatifu azichunguze nia zenu kwa Neno, mtakubaliana na Ujumbe huu. Mwache Kristo, Neno lililotiwa mafuta, aichunguze dhamiri yako. Hebu na aingie ndani yako, uone kama hilo ni Kweli ama si kweli. Na hilo ni jambo moja tu ama mawili ninayotaja, wakati kuna mamia ya hayo.

180 Je! Biblia inakubaliana na mwanamke kukata nywele zake? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Je! Biblia inaamini, inakubaliana na matatu, mabatizo katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu"? ["La."] Hakuna kitu kama hicho. Je! Biblia inakubaliana na mwanamke kuvaa nguo za mwanamume? ["La."] Vema, hebu chukua hayo mambo matatu hapo, wakati kuna mamia zaidi. Chunguza hilo katika Nuru ya Neno la Mungu.

181 Unasema, "Mimi ni mfuasi wa kanisa." Ndivyo alivyokuwa Kaini. Ndivyo Hawa alivyokuwa. Biblia inabashiri, katika siku za mwisho, ya kwamba Laodikia itakuwa jinsi iyo hiyo.

182 Hebu mwache Roho Mtakatifu aichunguze dhamiri yako, nawe utakubaliana na Danieli 5:12. Wakati yule malkia alipokuja mbele ya Belteshaza, na akasema aligundua kwamba kulikuwako na nabii, Danieli, alikuwa miongoni mwao, naye alikuwa ndiye mtanguzi wa mashaka. Mruhusu Roho Mtakatifu. Yeye ndiye nabii wa wakati huu. Hebu mruhusu aingie moyoni mwako sasa hivi na achunguze kwa Neno la Mungu, na mashaka kuhusu Ujumbe yataondolewa. Yeye hutangua mashaka yote. Chunguza uone, liko kwenye Neno la wakati huu kabisa.

183 Huwezi kuhubiri ujumbe wa Luther siku hizi. Ni sehemu Yake, bali huo ni miguu. A-ha. A-ha. Huwezi kuhubiri wa

Wesley. Huwezi kuhubiri wa Kipentekoste. Tuko mbali sana na hayo. Wao waliunda madhehebu na wakafa. Wao ni shina.

184 Shina liliota pamoja na jani, hiyo ndiyo hali ya kwanza ya kanisa. Sasa, hilo hapo halionekani kama punje ya kwanza iliyoingia ardhini, ile ngano.

185 Ya pili kutokea ni mbelewele. Hiyo bado haionekani kama ile punje. Inafanana zaidi nayo. Inaendelea kupata sura ya punje halisi. Bali hayo majani kwa kweli hayaonekani kama ile punje iliyoingia ardhini. Ni bebaji la uhai uliokuwa kwenye ile punje. Lakini ilifanya nini? Iliunda madhehebu, kama tu vile maumbile mengine yote yanavyoafikiana na jambo hili. Ilikufa.

186 Ndipo nini? Uhai ulipanda moja kwa moja ukaingia kwenye kishada. Kishada kina vijimpira vidogo-vidogo vingi sana vinavyoning'ining'inia juu yake, vinavyoonekana kama punje ndo—ndogo ndani yake. Inaonekana kana kwamba ni punje halisi, bali siyo.

187 Ndipo inashuka inaingia kwenye kapi. Ndipo inatoa kitu gani? Kapi.

188 Sasa, hebu chukua punje ya ngano, wakati ngano inapotokeza mara ya kwanza. Na Yesu alisema, "Punje ya ngano . . . " Basi hebu chukua ngano hiyo na uifungue. Uliivuna toka kwenye hilo shina. Ukaiangalia. Unasema, "Tuna punje ya ngano." Kuwa mwangalifu. Ni kama punje kabisa, bali hakuna punje hata kidogo ndani yake. Ni kapi.

189 Hao hapo Wapentekoste, "Wanafanana sana," kama vile Mathayo 24:24 ilivyosema, "ingewapoteza walio Wateule katika siku za mwisho, kama yamkini." Lakini ondoa ganda kwa ganda, huna punje hata. Punje iko huko nyuma ndani kabisa. Unaona?

190 Ndipo basi uhai unatoka kwenye hilo dhehebu, unaingia kwenye punje. Ndipo kitu gani kinatendeka? Punje inapoanza kukua, na kuwa kubwa hata inaweza kufunika kitu fulani, hayo madhehebu yanajitenga Nayo. Ni kwa nini hatuna madhehebu kutoka kwenye Huu? Hayatakuwako kamwe. Ni punje. Haiwezi kuendelea mbele zaidi. Tuko katika wakati wa mwisho. Kwa hiyo inapaswa kufanya nini sasa? Kukaa katika uwepo wa Mwana ipate kuivishwa, hiyo ni kweli kabisa, Neno lipate kuivishwa moyoni mwako, lipate kuzaa na kuishi kile tunachonena habari zake. Naam, bwana.

191 Ndipo hutakuwa na shaka tena, ukimruhusu Roho Mtakatifu akufunulie Hilo, kama vile yule malkia alivyosema juu ya Danieli.

192 Huenda ukasema, "Haya yote yana uhusiano gani na kutoa shukrani? Unazungumza juu ya kitu gani, Ndugu Branham? Hii hapa, saa tatu kasorobo. Hukusema kitu juu ya kutoa shukrani." Ni ujumbe wa jinsi gani kwa wakati huu, kwangu mimi! Naam, kweli.

193 Wale baba zetu wasafiri walikuwa na shukrani sana walipopata njia mpya ya maisha yao. Wakiisha kutenganishwa na madhehebu ya kale ya Uingereza na zile kanuni za imani, wangeweza kujifunga na Neno jipya, lililotiwa mafuta la wakati wao; hiyo ni kweli, Neno jipya, lililotiwa mafuta la wakati wao, kwa ajili ya siku zao.

194 Vivyo hivyo nasi tunaweza kutoa shukrani, kama wasafiri, kama Ibrahimu, tukiisha kujitenga na mambo ya ulimwengu, jamaa zetu wote. Ibrahimu alikuwa msafiri. Mungu ametutenganisha na dini zote zisizo hai. Ninazungumza kote nchini sasa, kanuni zote za imani zilizokufa. Na kuingia wapi? Ametutenga, na kutufungulia nchi mpya, Ujumbe mpya kwa ajili ya siku hii.

195 Pentekoste ilikauka na ikafa, kama Luther, Wesley, na hao wengine. Si chochote tena zaidi ya kundi la makanisa yaliyokusanyika pamoja. Wamo watu wazuri ndani mle, hata hivyo, nao wanapaswa kutoka.

196 Yeye alifanya nini? Alifungua ile Mihuri Saba ya Ujumbe wa mwisho. Unaona jambo hilo? Ile Mihuri Saba, ambayo, siri zote za nyakati saba za kanisa zilitiwa muhuri kwa Mihuri Saba. Wale watengenezaji hawakuwa na wakati wa kufanya hivyo katika siku zao. Hawakuishi muda mrefu vya kutosha. Bali huu ufunuo uliobarikiwa wa Mihuri Saba, umefunguliwa kwetu katika siku hizi za mwisho, kutokana na unabii ulioenda Arizona.

197 Jinsi nilivyomwomba Mungu, hivi majuzi, "Unafanya nini na mimi huku nje kwenye jangwa hili?"

198 Je! ulijua Musa aliandika Agano Jipya. . .ama Agano la Kale? Hakika aliliandika. Vitabu vinne vya kwanza vinatoa torati, kila kitu; Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati. Yeye aliandika Agano la Kale. Ili afanye hivyo, ilibidi awaache washirika wake wote na wapenzi wake, na aende nyikani.

199 Paulo aliandika Agano Jipya. Hiyo ni kweli. Aliandika Warumi, na Warumi na hizo zingine zote zilizo pale, Waebrania na Timotheo, na kadhalika. Na ili kufanya jambo hilo, ilibidi ajitenge, na ashuke aende huko Arabuni, jangwani, kwa muda wa miaka mitatu, akapate ufunuo wa Mungu.

200 "Loo," unasema, "vipi kuhusu Mathayo, Marko, Luka, na Yohana?" Wao walikuwa ni waandishi walioandika tu yale Yesu aliyofanya.

201 Paulo alitenganisha na akaliweka Neno pamoja. Hiyo ni kweli. Vema, basi, angalia, kama ilitakiwa kufanya hivyo, na ikabidi waende nyikani, mbali na wapenzi wao . . .

202 Je! mnakumbuka ninii, *Ni Wakati Gani, Bwana?* Ni wangapi waliopata kuusikia? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema,

"Amina."—Mh.] Je! ulikuwa ni sahihi kabisa? ["Amina."] Basi tuna ufunuo katika siku hizi za mwisho, kwa ajili ya Ujumbe wa Bwana Mungu kumkusanya Bibi-arusi Wake pamoja. Hakuna wakati mwingine ambao umeahidiwa hilo. Imeahidiwa katika wakati huu: Malaki 4, Luka 17:30, Yohana Mtakatifu 14:12. Yoeli 2:38. Ahadi hizo ni kama tu vile Yohana Mbatizaji alivyojitambulisha katika Maandiko.

203 Yesu alijitambulisha Mwenyewe. Wao walisema nini? "Hatumtaki mtu kama huyo!" "Yohana ni mshamba." Kanisa halikuweza kuupokea. Hicho ndicho kielelezo. Wala kanisa halitaupokea leo.

204 Lakini, kwa Wateule, Mungu anawaita Wateule. Wanajua jambo hilo: anamwita Bibi-arusi mwadilifu, lile Neno, Kanisa la siku za mwisho, Bibi mteule wa Bwana wetu Yesu Kristo, Neno. Kama . . . Yesu ni Neno. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Basi, Bibi-arusi daima ni sehemu ya Bwana Arusi, kwa hiyo Bibi-arusi hatakuwa madhehebu. Itabidi awe ni Neno, lililodhihirishwa, apate kuwa Bibi-arusi wa Kristo. Aliahidi kufanya jambo hilo. Alisema jinsi alivyofanya. Kamwe hatumii . . . hapotezi mpangilio Wake. Daima alifanya jambo hilo kwa mpangilio. Alilifanya, kila wakati, kwa mpangilio. Analifanya tena, akimwita Bibi-arusi Wake mwadilifu katika siku ya mwisho, Rebeka wa kupendeza akimngojea Isaka Wake. Ni wakati mzuri jinsi gani!

205 Hapa linaonyesha wazi, vile vitabu viwili ambavyo vitakuwa ni vya siri kwenu mtakaposoma kitabu cha *Nyakati Saba za Kanisa*. Vile vitabu viwili: Kitabu cha Uzima, kilisema, mtu mmoja anasema unaweza kuandika jina lako humo, hufutwi kamwe; mwingine anasema unaondoa jina lake kutoka katika Kitabu cha Uzima. Hili linaliweka dhahiri kabisa, papa hapa. Nitakoma kwa dakika chache, labda, kwenye mihtasari michache hapa, na mshike jambo hili kabla hatujafunga.

206 Uzima ni kitu kitakatifu, kwa Mungu, na umeandikwa katika kitabu. Mungu ndiye mwazilishi wa uhai. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

207 Maisha yetu ya kawaida hapa, tuliyo nayo, ni upotovu tu. Kwa kweli yanapaswa kuwa ni maisha mema, kwanzia, bali yamepotoshwa na kuzaliwa kwetu kwa kimaumbile. Uzima wa kwanza, ama muungano wako wa kwanza, wewe uliunganishwa wakati wa kuzaliwa, kwa maumbile, tendo la kawaida. Mtu wa kawaida alishirikishwa, mwanamume na mwanamke pamoja, walishirikiana katika kujuana kimwili, jambo ambalo liliyaleta maisha yako ya kwanza hapa, na hayo yanahusika na dhambi na mauti. Unawezaje kukosa kuona ule uzao wa nyoka?

208 Unapomwona mwanamke, zaotuka; hakuna jike lingine kama yeye; lililoumbwa kwa jinsi hiyo, akijua ya kwamba angeweza kudanganywa. Mungu alijua. Kama hakujua mwisho

tangu mwanzo, basi yeye hakuwa Mungu. Kama yeye hana kikomo, kama hana . . . Na hawezi kuwa asiye na kikomo bila ya kuwa mwenye kujua mambo yote, aliye kila mahali, ajuaye mambo yote, wa Milele. Kwa hiyo Yeye alijua mambo yote, Naye ilibidi amwumbe huyo mwanamke.

209 Huyo mtu hakuwa na mke. Mke na mume walikuwa ni mtu mmoja. Mwanamume alikuwa na roho ya kike na ya kiume ndani yake.

210 Ilibidi awatenganishe, achukue zaotuka, baada ya viumbe vyote kuumbwa. Hakuna jike lililoumbwa na Mungu, katika ule uumbaji wa asili, linaloweza kufanya kitu kama hicho. Mwanamke aliumbwa hivyo, apate kulitenda. Yeye alijua mwanamke angefanya hivyo. Kama hakujua, Yeye hakuwa Mungu.

211 Lakini, unaona, zile sifa zilizo ndani ya Mungu ilibidi zionyeshwe. I—ilibidi awe Mwokozi. Na ili kukifanya kila kitu kuwa kikamilifu, jinsi alivyokuwa amelipanga, basi kusingekuwako na kitu chochote ambacho kingepotea. Loo, msiwe watoto. Iweni wanaume na wanawake. Tuko kwenye mwisho wa safari. Angalia.

212 Sasa, ilikuwa ni maumbile, yaliyohusishwa na mauti. Mumeo wa kwanza, aliyekuwa anakutawala, alikuwa ni tabia yako iliyotokana na kuzaliwa kimwili. Kimwili, unaipenda dunia kwa sababu wewe ni dunia, na u sehemu ya dunia. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Tamaa zako zilikuwa, kimaumbile, kuipenda dunia ambayo wewe u sehemu yake. Wewe u sehemu ya maumbile. Unaamini hilo? ["Amina."] Na hilo ndilo hilo jambo lako la asili.

213 Hiyo ndiyo sababu huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kujitenga; huna budi kufa kwa mume huyo wa kwanza. Huwezi kuishi na jambo hilo. Huwezi tu kusema, "Vema, nitamtaliki, na kumning'iniza hapa juu mpaka wakati huo." La, bwana. Hakuna kuandika talaka! Ni yeye afe. Asili ya dunia haina budi kufa. Kila chembe yake haina budi kufa. Huna budi kuunganishwa mara nyingine, tena, na Asili nyingine.

214 Jina lako la asili yako ya kwanza, ulizaliwa, na kuandikwa katika kitabu cha uzima. Na matendo yako yote yaliandikwa humo, pia. Kila kitu ulichofanya chini ya asili hiyo kiliandikwa katika kitabu, kinachoitwa kitabu cha uzima.

215 Unaona, katika Danieli, wakati alipokuja kwa "Yule Mzee wa Siku, Ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu. Elfu kumi mara elfu kumi waliambatana naye, kumhudumia; yu—yule Bibi-arusi. Na ndipo vitabu vikafunguliwa." "Na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima." Unaona? Kuna watakatifu walioko kule tayari, lile Kanisa, Bibi-arusi. "Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima."

216 Sasa, wewe, bali ulipotenganishwa na ndoa hiyo, kwa mauti ya kiroho: Tamaa yako ya kimaumbile ni kukata nywele zako. Tamaa yako ya kimaumbile ni kuvaa kuptura, kupodoa uso wako. Tamaa yako ya kawaida ni kuwa mwenye akili, mtu mwerevu, kujua jambo fulani vizuri zaidi kuliko huyo mtu mwingine. Hayo ndiyo Hawa alitaka. Hicho ndicho kitu hasa alichotaka.

217 "Vema, aisee! Maskini duni wee, mhubiri hoi-hoi, ati unasimama hapo na kuniambia? Mimi nina Ph.D, LL." Hiyo inakufanya tu uwe mbali zaidi na Mungu, kila wakati unapoongezea kitu kimoja. Unaona? Unaona? Hiyo ni hakika. Ni kweli. Unaona?

218 Hiyo ndiyo Hawa aliyochukua. Alidungwa mimba ya aina hiyo. Hivyo ndivyo kanisa lilivyo siku hizi, kwa shule za Biblia na wenye akili. Basi, angalia, kila mmoja anatofautiana na mwingine, mchafuko mkubwa kama tu vile Biblia ilivyosema, "Babeli."

219 Bibi-arusi anajua mahali anaposimama. Idadi yake ni ndogo sana. Hakutakuwako na wengi watakaookolewa; ni wachache sana, sana, sana. Unasema, "Vema, hapo, lilisema, 'maelfu.'" Naam. Lakini wametoka katika kipindi cha miaka elfu mbili, pia, kwenye kila kipindi walichotokea. Kamwe . . .

220 Wakati wa Luther na kundi hilo; na kisha nao wakafa, na wakaenda, wakaunda madhehebu; kisha Wesley; na ndipo wakaja wapentekoste, na kadhalika. Na matawi hayo yote madogo yaliyojitokeza ya Wabaptisti, Wapresbiteri, Wamethodisti, Wanazarayo, Wapilgrim Holiness, na kadhalika, unaona, matawi hayo yote yalitokea huko kama jani.

221 Lakini, unakumbuka, wakati lilipoanguka; na punje hiyo ikaanza kuiva, kwamba unakuta, kabla punje hiyo kuweza kuiva, kila kitu kwenye shina hilo hakina budi kiwe kimekufa. Haleluya! Je! hamwezi kuona mahali tunaposimama? Uhai umo kwenye punje tena. Ni kitu gani? Ni kama tu punje ile ile iliyoingia ardhini, Yesu yeye yule katika mfano wa Bibi-arusi, nguvu zile zile, Kanisa lile lile, jambo lile lile, Neno lile lile. Neno lile lile lililofyonzwa kupitia kwenye hizi na kutokea hapa, na kufikia kilele chake hapa. Na Uhai wote ule ambao ulipitia hapa, uliwachukua watu wake. Sasa unafikia kilele chake, kwa ajili ya Unyakuo. Nitazungumzia jambo hilo kesho usiku, ama kesho kutwa usiku, mojawapo, Bwana akipenda.

222 Vema, ulivunja ndoa yako ya kwanza, kwa mauti ya kiroho. Sasa umezaliwa mara ya pili, ama umeolewa tena, kwenye ndoa mpya ya kiroho; si ya maisha yako ya kimaumbile ya mambo ya ulimwengu, bali ni ya Uzima wa Milele. Chembe hai hiyo iliyokuwa ndani yako hapo mwanzo, ilikupata.

223 Sasa, kitabu chako cha zamani kimetoweka, pamoja na ndoa yako ya zamani. Sasa, jina lako kwenye chako cha zamani,

katika ninii chako . . . limehamishwa. Sasa, unasema, "Unataka kuniambia ya kwamba kitabu changu cha zamani . . . " Mungu alikiweka kwenye Bahari ya Usahaulifu Wake. Unasimama mkamilifu mbele za Mungu.

224 Sasa, jina lako sasa liko kwenye Kitabu kipya; si kitabu cha uzima, bali kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kile Mwana-Kondoo alichokomboa. Si kile kitabu cha zamani cha ndoa yako ya kawaida, bali ndoa yako mpya, Bibi-arusi. Haleluya! Uhai wako mpya umo ndani ya Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, cheti chako cha ndoa, haleluya, ambapo chembechembe yako ya kweli ya Milele, tangu mwanzo, inakaa. Sasa si kwamba tu umesamehewa, bali umehesabiwa haki. Utukufu! "Kuhesabiwa haki," Warumi 5:1 ilisema. Naam. Warumi 5:1 ilisema, "Kwa hiyo tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani."

225 Chunguza neno hilo. Neno hilo halimaanishi kusamehewa. Neno hilo linamaanisha kuhesabiwa haki. Halimaanishi umesamehewa.

226 Kwa mfano, ulisikia nililewa pombe na—na kufanya mambo maovu, na kila kitu. Ndipo wewe unakuja, unaniambia. Ulikuta kwamba sikufanya hayo, ndipo unakuja huku, unasema, "Ndugu Branham, ninakusamehe." Ati unanisamehe? Sikufanya hayo, kwanza. Unaona?

227 Sasa, kama kweli nilifanya hayo, nina hatia. Lakini ungeweza kunisamehe, nami nisingekuwa na hatia. Lakini hata hivyo sijahesabiwa haki, kwa sababu kwa kweli nilifanya jambo hilo.

228 Lakini hilo neno, *kuhesabiwa haki*, ni kama kwamba hukufanya jambo hilo kamwe. Amina. Hata haliwaziwi, hata kidogo. Inafanywaje? Liko katika Kitabu cha Mungu cha Bahari ya Usahaulifu, kitabu chako cha kale na ndoa yako vimetalikiwa na vimekufa, na hata hayamo kwenye kumbukumbu za Mungu. Amina. Umehesabiwa haki. "Kwa hiyo tukiisha kuhesabiwa haki." Lilishtakiwa. Ulishtakiwa. Hukufanya jambo hilo kamwe, kwanza. Ile ndoa ya zamani iko kwenye Bahari ya Usahaulifu wa Mungu. Hukuolewa kwake, jambo la kwanza. Yeye, Bwana Arusi, alibeba aibu yako, Yeye Mwenyewe, kwa ajili yako, mahali pako. Yeye alipachukua mahali pako, kwa kuwa ulichaguliwa tangu zamani kwa ajili Yake, upate kuwa katika Bibi-Arusi Wake, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Biblia ilisema jambo hilo. Wewe ni Mbegu iliyochaguliwa tangu zamani.

229 Ulikujaje kufanya jambo hili? Ulidanganywa kwenye jambo hilo na ndoa yako ya kwanza, kwa mzazi wako mzinzi, Hawa. Si kosa lako wewe mwenyewe. Kwa kuzaliwa kwako kimaumbile, ulitokana na Hawa, aliyefanya uzinzi. Hiyo ndiyo sababu ulizaliwa mzinzi. Wewe ni mwenye dhambi, jambo la kwanza. Hiyo ni kweli. Ulidanganywa ukaingizwa humo. Hukuwa na . . . La, wewe, si kosa lako.

230 Kamwe hukufanya jambo hilo. Kwa sababu, hiyo chembe hai ndogo iliyokuwa ndani yako, ilikuwa iwe ni wewe, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu aliweka jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.

231 Ni kama ile hadithi yangu ndogo ya tai, ninyi nyote mmeisikia. Kuku. . . Mkulima mmoja mzee alimwatamisha ku—kuku, wakati mmoja. Kwa hiyo hakuwa na kuku wa kutosha kule. . . mayai ya kumwekea kuku huyo. Kwa hiyo basi alipata yai la tai, nao wakaliweka chini yake. Wakati yule tai alipozaliwa, alikuwa ni kifaranga wa kuchekesha sana hao vifaranga waliyepata kumwona, maskini tai mdogo akitembea-tembea. Naye kuku angelia, "Chu, chu, chu, chu."

232 Maskini yule kifaranga wa tai akasema, "Sijui kitu hicho kinaliaje, lakini ninamfuata, haidhuru."

233 Ndipo wakatoka kwenda huko nje kwenye eneo linalozunguka banda na kuanza kuchakura kwenye malundo ya mbolea. Akaita "Chu, chu, chu." Hiki ni kizuri. Hiki ni kizuri. Jiunge na letu. Na hii ndiyo ninii . . . "

234 Maskini kifaranga hicho cha tai, kisingeweza kula takataka hizo. Unaona? Yeye alininii tu—alifuatana tu na hao kuku kwa sababu hakujua. Hakujua la kufanya. Na ndipo akatoka akaenda huko, naye angepata *hiki* ama *kile*. Ndipo maskini huyo tai mdogo alininii tu. . . Ilimbidi tu kuvumilia jambo hilo, bali ha—hakujua jinsi ya kulifanya. Lakini alikuwa amewaona hao kuku wote wakifanya hivyo, bali kuna kitu fulani tofauti. Yeye hakupenda jambo hilo.

235 Kwa hiyo, siku moja, mama yake alijua ya kwamba alikuwa ametaga mayai mawili. Kwa hiyo akaanza kulitafuta hilo lingine, akaruka kila mahali, akitafuta, kama vile Roho Mtakatifu mkuu. Siku moja aliruka juu ya lile banda, hilo dhehebu. Akaangalia kule chini, naye akamwona mtoto wake mchanga. Akapaza sauti. Ilikuwa ni Sauti ya kitu fulani kilichotoa mwangwi kutoka ndani yake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Loo, Hiyo inanivutia! Loo! Hebu acha chembe hai halisi iliyozaliwa kwa kuchaguliwa tangu zamani, iliyochaguliwa tangu zamani na Mungu, isikie Neno la Mungu, Hilo ni muziki kwake. Anajua kwamba ni Kweli.

236 Yeye amechoshwa na upuuzi huo wa kimadhehebu, hata hivyo, "Jiunge nasi. Njoo, uambatane na sisi. Tuna karamu ya kirafiki. Tuna *hili*. Tuna . . . " Kamwe haikusikika kwamba ni sawa, kwa jamaa huyo mdogo.

237 Akasema, "Mwanangu, wewe si wa kikundi hicho, kwa vyovyote vile. Wewe ni wangu. Wewe u wangu."

238 Akasema, "Mama, hilo linasikika ni halisi. Nitatokaje?"

239 "Hebu ruka tu. Nitakushika." A-ha. Hivyo ndivyo inavyokupasa tu kufanya.

240 Neno lililotiwa mafuta la Mungu likithibitishwa mbele ya mtu yeyote aliyezaliwa awe Mwana wa Mungu, akiwa na chembechembe hai ndani yake iliyochaguliwa tangu zamani kwa ajili ya wakati huu, atauona Ujumbe wa Mungu hakika tu kama vile kulivyo na Mungu Mbinguni. Martin Luther aliliona kwa wakati wake. Wesley aliliona kwa wakati wake. Mpentekoste aliliona kwa wake. Sasa na wewe je? Aa-ha. Hao waliingia katika dhehebu. Hili hapa Neno likilihukumu; likiwaambia kile tunachopaswa kuwa nacho leo, na ni Malaki 4 hasa na ahadi hizi nyingine zote za wakati huu. Unaona kitu gani? Unaangalia kitu gani? Amina. Tumewasili. Tai halisi, wa kweli husikia. "Kondoo wangu huisikia sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata."

241 Kwa nini? Liliwekwa mle ndani kwa kuchaguliwa tangu zamani. Ulichaguliwa tangu zamani kuwa mwana wa Mungu. Ulikuwa ndani ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Umedhihirishwa tu katika siku hii kwa ajili ya heshima na utukufu Wake. Unawezaje kufanya jambo hilo bila kuliheshimu Neno Lake, na kusimama na kila Neno la Mungu? Naam, bwana. Ambapo, wewe ni sehemu ya Neno hilo, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Kwa sababu, angalia, Mungu ni Neno. Unaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, basi, kama . . . Yeye daima alikuwa ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno." Na kama Neno lilikuwa ni Mungu, basi wewe ulikuwa ndani ya Mungu. Neno, sehemu unayopaswa kutimiza, ilikuwa ndani ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alikuona. Alikujua. Alikuchagua tangu zamani kwenye sehemu hiyo.

242 Ninakwambia, kama tu vile yule tai alivyoitambua ile sauti, vivyo hivyo na Mkristo ha—halisi, aliye—aliyezaliwa mara ya pili huitambua Sauti ya Mungu akizungumza kupitia kwenye Neno, wanapoliona limetiwa mafuta na kuthibitishwa. Angalia. Yeye aliangalia Huko *Juu*. Hakumwona maskini kuku huyu akiita chu-chu *hapa*, "Jiunge na sisi na uende *hapa*. Na uendee *hili*, na uende kwenye *hili* na *lile*." Aliona ki—kiumbe kama kile alichotaka kuwa, kikiruka hewani, kikipiga kelele, kiko huru, huko juu kabisa, juu ya koho wote na mambo ya duniani. Haleluya! Alitaka kuwa hivyo kwa kuwa kitu kilikuwa ndani yake kuwa hivyo.

243 Na mtu aliyezaliwa na Mungu, mwana wa Mungu, hana budi kuwa na tabia ya Mungu. Hana budi kuwa kama Mungu. Yeye humheshimu Mungu. Yeye ni sehemu ya Neno la Mungu. Na katika siku hizi za mwisho, za Bibi-arusi huyu akichukua umbo, nguvu zile zile hasa Yeye alizokuwa nazo hapo mwanzo, zimekuja kupitia kwenye madhehebu haya, na kadhalika, na zimetokea kwa ajili ya Bibi-arusi. Bwana Arusi hawezi kuwa kitu kingine chochote ila hicho.

244 Walipaswa kuona Hilo, hao Wayahudi katika siku zao, wakati walipoliona limedhihirishwa pale mbele zao, kama

vile nabii alivyosema Yeye alikuwa. Alisema, "Yachunguzeni Maandiko; ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Hayo ndiyo yanayonishuhudia. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, msiniamini. Lakini ingawa hamwezi kuniamini Mimi, hebu amininі kazi ambazo nimefanya."

245 Wakasema, "Baba zetu walikula mana jangwani kwa miaka arobaini. Sisi tunajua tulipo."

246 Akasema, "Na kila mmoja wao amekufa," hiyo ni kusema, wametengwa Milele. Kila mmoja alikufa. Kulikuwa na watatu peke yao, wawili waliotoka katika milioni moja, milioni mbili. Hiyo ni kusema mmoja katika milioni moja.

247 Mbona, kuingizwa mbegu, mbegu kutoka kwa dume na jike, kwa kawaida kuna yai moja rutubifu. Kuna yai moja, mbegu moja rutubifu, kama umeshaona kule kuzalishwa kwa mbegu katika ng'ombe. Angalia. Haya *hapa* mayai mi—milioni moja; hizi *hapa* mbegu zazi milioni moja; na wakati zi—zinapotolewa, zipate kukutana pamoja kwenye tumbo la uzazi, zikipita kwenye tyubu na kuingia tumboni, zinakutana. Moja ya hizo ni mayai. Mayai milioni moja; mbegu milioni moja. Kuna yai moja tu mle ndani rutubifu. Kuna mbegu moja tu rutubifu. Zote ziko hai. Unaweza kuwaangalia hao ndama wadogo wakichezacheza mle ndani, chembe ndogo sana ambayo ungeweza kuweka kwenye kijiti cha kiberiti.

248 Na Demos na hao wengine wanasikiliza usiku wa leo, naye anakumbuka wakati tulipowachukua. Yeye alinipeleka kule chini, akanionyesha jinsi kitu hicho kilivyofanya kazi. Tyubu za majaribio, na unatia ndani za kutosha tu ambazo ungeweza kuziweka kwenye ncha ya kijiti cha kiberiti. Mle ndani mlikuwamo na maelfu ya ndama wadogo na mafahali, bali ni mmoja wao tu anayeweza kuishi. Mmoja wao tu! Na hili hapa bonge lao kubwa, *hapa*. Na utaona, mmoja atatambaa atoke kati ya huyu *hapa*, apande juu moja kwa moja, mbegu hiyo inakuja *hapa*; na yai fulani litatoka miongoni mwa mayai haya mengine upande *huu*, na yatakutana. Ndipo hayo yaliyosalia yanakufa. Hata hivyo, yako hai, bali yanakufa.

249 Kwa sababu, kuna Kitu fulani, Mtu fulani alililifanya *hili* rutubifu, na kulichagua *hili*, pia. Ni kukusudiwa tangu zamani, ndugu yangu. Hakika. Inabidi Mungu aamue ama atakuwa ni mvulana au msichana, mwenye nywele nyekundu, nywele nyeusi, ama chochote kile. Linaamuliwa na Mungu. Ni fumbo kubwa kuliko uzazi wa kibikira, kwangu mimi. Lakini, hebu angalia, yaliyosalia yanakufa.

250 Kulikuwako na watu milioni mbili waliotoka, wakaimba, wakapaza sauti, wakafanya kila kitu. Wakanena kwa... hawakunena kwa lugha kamwe. Bali walipaza sauti, na—na kumtukuza Mungu, na kucheza huku na huko baharini, na kufanya kila kitu ambacho hao wengine wote walifanya, bali

kulikuwako na wawili tu walioingia katika nchi ya ahadi. Kalebu aliingia, Kalebu na Yoshua, wawili peke yao. Hiyo ni kusema mmoja katika milioni moja. Ni mmoja katika milioni moja katika uzazi wa kawaida. Kila mmoja wao alikuwa na baraka zile zile.

Loo, enyi Wapentekoste, natumaini hamtaamka mkiwa mmechelewa kupita kiasi.

251 Mmoja katika milioni moja. Angalia. Inakisiwa kuna milioni mia tano ya wanaodhaniwa kwamba ni Wakristo ulimwenguni leo hii. Kama Yesu angekuja, kungekuwako na mia tano tu ambao wangeenda pamoja Naye, basi, kama takwimu hiyo ingekuwa sahihi. Mbona, kuna zaidi ya hao wanaokosekana kila siku, kote ulimwenguni. Hawajui lolote juu ya jambo hilo.

252 "'Ninafahamu,' walisema waandishi, 'unajua ya kwamba . . .' Mbona waandishi wanasema ya kwamba—ya kwamba, 'Imempasa Eliya kuja kwanza'?" Walimwambia Yesu.

253 Yeye akasema, "Eliya amekuja tayari wala hamkujua." Mnaona? Yeye alitenda sawasawa na vile Maandiko yalivyosema yangempata Yeye. Mnaona? "Vivyo hivyo imempasa Mwana wa Adamu kuteseka. Chini . . . " Hawakumtambua. Hata hivyo, wote walikuwa kanisani. Wote walidai kwamba wako hai.

254 Na hebu tu mwache Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili, mtumishi halisi wa Mungu, asikie hilo Neno la Mungu, atatoka moja kwa moja kupitia kwenye kila madhehebu, aingie kwenye hilo shamba halisi lenye rutuba, kwa Neno, tuta la kupanda mbegu. Atafanya tu hivyo. Sijui jinsi anavyofanya jambo hilo. Mungu amelikusudia lifanywe.

255 Ulidanganywa hapo mwanzoni, na ndoa yako ya kwanza. Sasa unajua yaliyo kweli. Kama tu nilivyosema, maskini yule tai mdogo aliposikia Sauti ya Bwana Arusi, alienda Kwake, Neno la Mungu lililotiwa mafuta, lililothibitishwa kwa ajili ya siku hizi za mwisho.

256 Nuhu alikuwa ndiye Neno lililothibitishwa la wakati wake. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, ujumbe wake hautafanya kazi siku hizi.

257 Musa alikuwa ndiye Neno lililothibitishwa la wakati wake. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Halitafanya kazi kwa sasa. Yesu alikuwa . . .

258 Yohana alikuwa ni Neno lililothibitishwa. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Lisingefanya kazi katika siku za Yesu. Bila shaka halingefanya kazi. La, bwana. "Torati na manabii walikuwapo mpaka Yohana; tangu wakati huo, Ufalme wa Mbinguni."

259 Mitume, hao walioiandika Biblia. Huyu hapa Luther anatoka, katika matengenezo, maneno yake, ya kwamba,

kanisa lake, halitafaa kitu leo. La Wesley halitafaa kitu. La Kipentekoste halitafaa kitu. Lilifaa katika siku zao.

260 Lakini ni siku nyingine. Huku ni kufunguliwa kwa Mihuri Saba. Ninajua linasikika la kigeni kwenu, bali Mungu amelithibitisha kikamilifu sana. Hakuna ninii—hakuna swali katika jambo hilo. Ni kamilifu tu! Siyasambazi hayo kwa ajili ya kusanyiko la mahali hapa. Ninawazungumzia watu kote nchini. Mnaona? Fanyeni mtakalo.

261 Sasa angalia Neno lililotiwa mafuta la siku yake, ambalo ninyi ni sehemu yake, kwa kuchaguliwa tangu zamani. Mara moja wewe, kama kwamba, ulijua. Wakati ulipolisikia Hilo, ulitambua upesi sana ya kwamba wewe ulikuwa tai. Pia ulitambua ya kwamba hukuwa kuku wa kimadhehebu, jambo la kwanza. Ulijua kuna kasoro fulani mahali pale. Kuna kasoro, hiyo ni kweli, kwa kuwa unajua ya kwamba ulinaswa katika kitu hicho, hapo mwanzoni.

262 Yeye, Bwana Arusi, alikuondolea aibu yako, "Na kuiweka katika Bahari ya Usahaulifu, kwa kuoshwa kwa Maji ya Neno na Damu ya Uzima." Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Mume wako wa kwanza aliyekuoa, ulimwengu; yule Bwana Arusi aliyetiwa mafuta, aliyekuchagua tangu zamani, amakuosha kwa kuoshwa kwa Maji. Kwa "kanisa"? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Hilo halisikiki kuwa sawa. Sivyo? ["La."] Unaweza ukapata hilo kwenye mtungo wa mwaka, bali si katika Biblia ya Mungu. "Kwa kuoshwa kwa maji kwa Neno." Katika Neno! Unaona? Kwa ninii . . .

263 Umesimama ukiwa umehesabiwa haki kabisa, kana kwamba hujawahi kamwe kufanya jambo hilo hapo mwanzo. Huo ndio Ujumbe wangu kwa Kanisa sasa. Unaponinii . . . tunapoondoka hewani, sasa hivi tu. Unasimama, kama unasimama kwenye Neno la Mungu na ukishikilia Neno la Mungu, kila amina, kila yodi, kila nukta. Unasimama wapi? Ninajaribu kuwaambia, ondokeni kwenye hayo makapi. Na mtoke mwingie hapa kwenye ngano, ambapo mnaweza kuiva mbele za Mwana. Ninasikia kuja kwa kivuna nafaka. Mmesimama mkiwa wakamilifu, waliohesabiwa haki, kana kwamba kamwe hamkutenda jambo hilo hapo kwanza. Haleluya!

264 Nena kuhusu kutoa shukrani! Ninajisikia vizuri kweli. Ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo kuliko chochote ninachojua.

265 Ninyi ni Bibi-arusi msafi, asiye na waa, asiye na dhambi, wa Mwana wa Mungu aliye hai. Kila mwanamume na mwanamke aliyezaliwa na Roho wa Mungu, na kuoshwa katika Damu ya Yesu Kristo, na anaamini kila Neno la Mungu, anasimama kana kwamba hakuwahi kutenda dhambi kwanza. Wewe ni mkamilifu. Damu ya Yesu Kristo! Unawezaje . . . Kama mtu . . .

266 Kama nilipaswa kufa asubuhi, mtu fulani akapachukua mahali pangu, siwezi kufa kwa ajili ya dhambi hiyo. Mtu fulani alipachukua mahali pangu.

267 Naye Yesu, aliye Neno, alipachukua mahali pangu. Alifanyika mimi, mwenye dhambi, nipate kuwa Yeye, lile Neno. Amina. Hebu niwe mwaminifu Kwalo, si kwa kanisa. Neno! Amina.

268 Loo, huo muungano wa kiroho wa Kristo na Kanisa Lake sasa, wakati mwili unapofanyika Neno, nalo Neno linafanyika mwili, linadhihirishwa, linathibitishwa. Vile vile hasa Biblia ilivyosema ingetendeka katika siku hii, inatendeka, siku baada ya siku. Mbona, inalundikana upesi sana huko nje, katika yale majangwa, na mambo yanayotendeka, hata nisingeweza kufuatilia jambo hilo. Tuko karibu na kule Kuja kwa Yesu, kuunganishwa na Kanisa Lake, ambapo Neno linafanyika Neno. Wito wa Roho Mtakatifu, akichunguza mioyo!

269 Unasimama, mkamilifu. Hukuwahi kutenda dhambi kwanza kabisa. Mungu hata hajui. Iko katika Bahari ya Usahaulifu. Hukuitenda kamwe. Ulituhumiwa hiyo, na yule mshtaki. Lakini kwa kweli, tangu mwanzo, ulichaguliwa tangu zamani kuwa mwana na kuwa binti ya Mungu. Umesimama pale, umeoshwa. Na kitabu chako cha kale cha talaka kimeondolewa, na kimekufa, hakiko kabisa, hata katika mawazo ya Mungu.

270 Wewe ni Bibi-arusi mwadilifu wa Kristo, aliyeoshwa katika Damu ya Kristo. Mwana wa Mungu wa thamani, mwadilifu, asiye na dhambi akisimama na Bibi-arusi Neno asiye na doa, asiyeghoshiwa, ambaye alimwosha kwa Maji ya Damu Yake Mwenyewe; aliyefanyika mwili na kudhihirishwa, apate kuwachukua ninyi mliochaguliwa tangu zamani awapeleke kwenye kifua cha Baba, kabla ya mwanzo, kama vile alivyokuwa Yeye. Yeye alikuwa ile sifa kuu ya Mungu, inayoitwa "upendo."

271 Chochote mlicho, ninyi ni watumishi wa Mungu, chochote Mungu anachokutaka ufanye, nafasi yako ilipo. "Mungu aliweka Kanisani, wengine mitume, manabii, waalimu, wachungaji . . . " Yeye aliwaweka hao kwa uwezo wa kuchagua Kwake Mwenyewe tangu zamani. Nawe ulikuwa hivyo, kwanza kabisa.

272 Ndoa yako ya kwanza ilifutiliwa mbali. Ilifutiliwa mbali. Hukuwahi kuifanya, jambo la kwanza. Kwa sababu, kuna kitu kimoja tu kingaliweza hufanya jambo hilo, hicho kingekuwa ni Mungu ashuke, Yeye Mwenyewe, na kupachukua mahali pako katika umbo la Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, na kukuosha kwa Maji, kwa kuoshwa kwa Maji kwa Neno. Neno; si madhehebu! Neno lilikuosha. Bali kama hutasimama katika Maji ya Neno, utapataje kuoshwa? Ungali una madoadoa kama Hawa alivyokuwa.

Ee, mpendwa Mwana-Kondoo unayekufa,
Damu Yako ya thamani
Haitapoteza nguzu Zake kamwe,
Mpaka Kanisa lote la Mungu lililokombolewa,
Litakapookolewa lisitende dhambi tena.

273 Dhambi ni kitu gani? *Dhambi* ni "kutokuamini." Kutokuamini katika (kitu gani?) Neno; kutokumwamini Mungu, ambaye ni Neno.

274 Wasafi, wasioghoshiwa; loo, haleluya; tunaondoka hivi karibuni kuelekea mbinguni; amina; tuko tayari. Wazieni. Mavazi yenu, yameoshwa kwa Maji ya Neno linalotoka damu! Neno lilifanyika Damu. Neno lilitoka damu kwa ajili yako, nawe umeoshwa katika Neno linalotoka damu. Neno, linalotoka damu! Uhai wa Mungu katika Neno, nalo Neno lilitoka damu kwa ajili yako, upate kuoshwa kutokana na uchafu wa hawa makahaba, na usafishwe na kutakaswa kwa kuoshwa kwa Maji ya Neno, na linafanya nia yako na moyo wako vitulie katika Mungu na katika Neno Lake.

275 Sasa, unajuaje jambo hilo ni kweli? Mungu anaposhuka na kulithibitisha na kulihakikisha.

276 Unasema, "Vema, sikuamini jambo hilo namna hiyo." Hawakuamini kwa Njia ya Yesu, lakini Mungu alilithibitisha. Hawakuliamini kwa njia ya Nuhu. Hawakuliamini katika njia ya Musa. Walikuwa radhi kuamini neno la Balaamu, "Sisi sote ni kitu kimoja, kwa hiyo hebu na tushirikiane pamoja."

"Jitengeni," Biblia ilisema, "na kutokuamini."

277 Haleluya! Sasa angalia. Wewe si hivyo tu ulivyo, bali unaenda kwenye Arusi huko mbinguni. Na umevaa utepe wa ndoa ya neema iliyokusudiwa tangu zamani, usiyostahili, utepe wa neema usiyostahili kwa nafsi yako. Mungu alifanya jambo hilo, Yeye Mwenyewe. Alikujua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa hiyo akakuvisha utepe wa arusi Pale, akaliandika jina lako katika Kitabu. Ni wakati wa kutoa shukrani jinsi gani! Haleluya! Mungu wetu asifiwe!

278 Sasa, katika kufunga, huenda nikasema hivi. Sote tunajua ya kwamba kanisa la kisasa, la Kipentekoste, katika hali yake ya sasa . . . madhehebu yote pamoja, nitayatupa yote kwenye tita moja, kwa sababu ndivyo yalivyo. Wewe kumbuka, Yeye atayafunga magugu matita, kwanza, kisha ayachome moto. Achukue ninii . . . Yeye atachukua mashina yote ya ngano na kuyachoma moto, kwanza; kisha atachukua, aje na kuichukua ngano Yake na kuipeleka Nyumbani. Wote wanakusanyika katika tita, tita la Wamethodisti, Wabaptisti, Wapentekoste, yote yakielekea kwenye Baraza la Ekumeni. Hivyo tu. Yote yanachomwa moto. Unaona?

279 Sote tunajua ya kwamba kanisa la kisasa, katika hali yake ya sasa na tabia yake ya sasa, halimo katika hali ya kutimiza lile

agizo kuu ambalo Mungu alilipa Kanisa kwa ajili ya siku hii. Ni Wapentekoste wangapi wanaoweza kusema "amina" kwa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kweli. Unaona? Liko katika . . .

280 Sisi ni wa umoja, wa uwili, wa utatu, *hili*, *lile*, *linginelo*, wanagombana, wanapigana. Mmoja ni *hiki*, na mmoja ni *kile*, na *kinginecho*. Na kila mmoja wao, anaogopa kukabiliana na Neno, moja kwa moja kufikia kwenye majaribio. Unaona? Wanajua. Ukiwaambia juu ya Hilo; wanasema, "Si—siwezi kujizuia. Siwezi kuamini Hilo. Sijali anafanya nini. Mimi . . ." Unaona? Unaona? Unaona? Inaonyesha una mama na baba wa aina gani. "Huenda ukawa mzee wa jimbo siku moja. Huenda ukawa *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*." Afadhali uwe mwana wa Mungu.

281 Sasa, tunajua ya kwamba kanisa lisingeweza, kanisa la Kipentekoste, hasha, hasha, halingeweza kutekeleza Ujumbe wa siku za mwisho, katika hali yake ya sasa. Je! lingeweza? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Mbona, hata haliwezi kukubaliana juu ya Neno moja ama mawili katika Biblia. Utautekelezaje? Haliwezi. Kwa hiyo, unaona, madhehebu hayahesabiwi. Hiyo ni kweli.

Itakuwa ni watu walioteuliwa ambao wameteuliwa kwa ajili ya jambo hilo. Unaona?

282 Unajua, na vivyo hivyo kila mmoja wetu anajua, ya kwamba safu nzima ya watu wa kimadhehebu, Wapentekoste na wengineo, wamekufa, yaani, kwa Mkristo wa Ujumbe aliyezaliwa mara ya pili. A-ha. Mume wako wa kwanza amekufa. Unajua ya kwamba amekufa. Mungu alimwacha afe. Imekwisha. Njia zake zote za kisayansi, kiakili, kielimu, kisayansi, zinazoitwa shule za Biblia na kadhalika zimeangamia. Limetenda kitu gani? Walitengana, wa umoja *hapa*, na wa utatu *hapa*, na wa uwili *hapa*, na upande huu *hapa*, na *hapa* chini, na ni machafuko makubwa sana, na wanajiita wenyewe Wapentekoste.

283 Mbona, nilienda kwa kijana mmoja, hivi majuzi; anasikiliza papa hapa ndani, sasa hivi. Na kijana mwanamke, yeye alikuwa ni mfuasi wa kanisa fulani. Akasema . . . Nikasema . . . Walitengana. Nikasema, "Kuna shida gani?"

Akasema, "Tuna imani tofauti."

Nikasema, "Loo, samahani. Je! wewe ni Mkatoliki?"

284 Akasema, "La." Akaniambia kanisa lake la kimadhehebu alilokuwa mfuasi wake, Mpentekoste.

285 Nikasema, "Na *lako* ni lipi?" Mvulana ni Mpentekoste, pia, bali ni wa dhehebu lingine. Loo!

286 Mnajua, kanisa Katoliki la Kirumi lilianza, likiwa la Kipentekoste? Ni wangapi wanaojua kwamba hilo ni kweli?

[Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Imelichukua muda wa miaka elfu mbili kufikia mahali lilipo sasa, halichukui kitu chochote cha Maandiko tena. Hata. Mbona, la Kipentekoste, katika miaka ishirini tangu sasa, litakuwa baya kuliko walivyo sasa, likiendelea jinsi linavyoendelea sasa. Mbona, ni hakika. Unaona? Ni kitu gani? Ni kitu gani? Angalia mama na baba yao ni nani. Wanawaachilia wanawake wao wakate nywele zao. Wanaweza kufanya karibu kila kitu wanachotaka kufanya. "Mradi tu ni wafuasi wa kanisa hili, hilo tu ndilo jambo muhimu."

287 Loo, si ajabu, si ajabu hukumu ya Mungu inajikusanya! Mungu aliweka jambo Hilo moja kwa moja mbele ya macho yenu na mnayafunga macho yenu na kukosa kuliangalia. Naam. Mnafunga mioyo yenu yenye huruma, wakati mnapoona Neno la Kweli la Mungu na hii Mihuri Saba ikithibitishwa na kuhakikishwa kwamba ni kweli. Na kushuhudiwa mbinguni, kote katika mataifa na popote pale, kwa ishara kuu na maajabu ambayo aliahidi angefanya, kisha mtu unajifungia, unasema, "Si—sijui. Si—siwezi kulizuia. Mimi . . ." Unaona? Loo, jamani! Limekufa, wala halijui. Dhambi na makosa! Wewe umekufa. Loo, jamani!

288 Sote tunajua ya kwamba kanisa likiwa katika hali hiyo lisingeweza kumalizia siku hii ya mwisho. Lingewezaje kuingiza Malaki 4 ndani? Lingewezaje? Hata hawaamini katika kitu kama hicho. Lingewezaje kuamini, kuingiza Luka 17:30 ndani? Lingewezaje kuingiza Maandiko haya mengine yote yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku hii ya mwisho? Lisingeweza kufanya hivyo, kwa kuwa linayakana. "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu."

289 Angalia hali ilivyo, Lutu, ambayo Sodoma ilikuwa ndani yake, katika siku hiyo. Angalia, hali ya kanisa la siku hii. Angalia kilichompata Ibrahimu, yule Mteule.

290 Angalia kilichompata Lutu na hao wengine huko Sodoma. Mwangalie huyo Billy Graham na Oral Roberts, hao huko chini miongoni mwa madhehebu hayo. Angalia Kanisa teule la Ibrahimu, lilijitoa nje.

291 Angalia ni ishara ya namna gani, ambayo Yesu Mwenyewe, Mungu aliyefanyika mwili akiwa amesimama pale katika mwili wa kibinadamu. Unasema, "Huyo alikuwa ni Malaika." Biblia ilisema alikuwa ni Mungu.

292 Bwana Mungu, Elohimu, akiwa amesimama pale katika mwili wa binadamu, akionyesha ya kwamba atalitia Kanisa Lake upako wa namna hiyo katika siku za mwisho. Itakuwa ni Mungu akitenda kazi katika mwili wa binadamu tena. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Adamu." Jambo lile lile. Wanayaona

papo hapo katika Maandiko. Soma ninii . . . "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa mnadhani ndani ya Hayo mna Uzima wa Milele." Na Hayo Ndiyo yanayoshuhudia jambo Hili. Mnaona? Mnaona?

293 Kwa hiyo tunajua wamekufa. Mungu aliliacha life katika mpango wake wa kibinafsi, wa kisayansi, wa kielimu.

294 Wapentekoste wote walikuwa na tabia ya kuzungumza juu ya—juu ya kuwapeleka watoto wao kwenye shule za Biblia, zamani wakati maskini Ndugu Loyate, na hao wengine walipokuwa hapa, nao wangewafukuza kanisani. "Lakini, loo, sasa ni jambo lililotukuka sana. Mwanangu yuko kwenye shule ya Biblia." Yeye anachimba kaburi lake. Kwa hiyo, sasa, unafikiri wangeweza kuvumilia Hilo, siku hizi?

295 Mnafikiri ninajaribu kuunga mkono ujinga? La. Ninawaambia kuna tofauti kati ya wakati huu wa kielimu tunaoishi, ambapo kanisa limetiwa mimba na sayansi na haya yote yanayoitwa "mambo yaliyowaziwa vizuri" na kila kitu. Humwazii Mungu.

296 Vema, hao—hao makuhani walikuwa wamemwazia Mungu kikamilifu kabisa. Walijua Masihi angekuja jinsi gani, bali Yeye alikuja tofauti sana na vile walivyokuwa wamemwazia. Halikuwa la kisayansi. "Mtu huyu angewezaje, akiwa ni Mtoto haramu? Alisoma wapi? Elimu Yake ilitoka wapi? Alipata wapi elimu hii?"

297 "Mbona, Wewe unajaribu kutufundisha sisi? Umezaliwa katika uasherati." Unaona? Loo, jamani!

298 Unaona jambo lile lile likijirudia tena? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona likijirudia tena? Yote katika sayansi yao ya kidini, sayansi yao ya kidini kulingana na vile shule yao ya Biblia ilivyosema, hivyo ndivyo wanavyolitaka Hilo. "Hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa, la sivyo jambo Hilo si kweli."

299 Mungu anawapumbaza tu, kila wakati. Daima linakuja vinginevyo. Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Nuhu; ilikuwa hivyo katika siku za Musa; ikawa hivyo katika siku za Kristo; ikawa hivyo katika siku za Yohana; ikawa hivyo katika siku za wanafunzi; ikawa hivyo katika siku za Wesley; ikawa hivyo siku za Luther; ikawa hivyo katika siku za Upentekoste; na hivyo basi imejirudia tena. Halibadilishi mpangilio wake. Daima inatokea vile vile. Ni watengenezaji tu katika zile nyakati saba, sita, mpaka wa saba. Na Ufunuo 10 ilisema, katika saa hii mambo yatabadilika. Na yalibadilika.

300 Sasa tunafunga, katika kusema hivi. Kumalizia lile agizo kuu, wangewezaje kulitekeleza? Tunajua wao wamekufa. Mungu amewaacha wafe katika wakati huu wa kisayansi, wote, ili—ili apate (kufanya nini?) kumfungulia Bibi-arusi wa Kristo asiye wa kimadhehebu ile siri ya Mihuri Saba. Madhehebu yanawezaje kuikubali hiyo Mihuri Saba, wakati iko kinyume kabisa, uzao wa

nyoka na mambo hayo mengine yote? Siri hizo zote saba, nzima, ni kinyume na vile walivyofundishwa, kwa kuwa waliamini ile shule ya kale kutoka kwenye shule yao ya Biblia.

301 Nayo ile Mihuri Saba ya Mungu, wakati ilipofunguliwa kule mlimani: Acha Mungu, hapana, acha nife sasa hivi kwenye mimbara hii kama hiyo si Kweli. Nami nilitangulia kuwaambia, mwaka mmoja na miezi sita kabla halijatukia, yale Yeye aliyoniambia, "Nenda Arizona," na kile ambacho kingetukia huko nje jangwani. Na wapo watu wanaoketi papa hapa, usiku wa leo, waliokuwa wamesimama papo hapo wakati wale Malaika saba waliposhuka. Na hata ga . . . Lile gazeti, gazeti la *Life*, liliandika makala Yake. Iko moja kwa moja kule kwenye chumba cha uchunguzi wa anga, kila kitu. Sasa hata hawajui hayo yote yanahusu nini.

302 Na kila kitu kimekwisha kusemwa, loo, hata kufikia kwenye maangamizi ya California, yanayokuja sasa, na mambo haya mengine yote. Na jinsi nilivyowaambia ingekuwa ni siku ngapi, jinsi itakavyokuwa ambapo tetemeko hili kubwa la nchi lilipotukia huko Alaska, na hilo lingekuwa ndio mwanzo wa ishara za wakati, na kile ambacho kingetukia. Na ilikuwa tu ni neno kwa neno, vile Ilivyosema, haijashindwa kamwe hata wakati mmoja. Hamjaliona kamwe likishindwa. Wala haliwezi kushindwa, kwa maana ni Maneno ya Mungu. "Na Mbingu na nchi zitapita, bali Hilo haliwezi kushindwa." Hiyo ni kweli.

303 Ilibidi Mungu afungue hiyo Mihuri Saba, si katika madhehebu fulani. Daima nimepinga kitu hicho. Lakini, nje ya madhehebu, huenda akachukua Bibi-arusi, sio bibi-arusi wa kimadhehebu. Asingeweza kufanya hivyo. Ni kinyume cha Neno Lake Mwenyewe. Yeye alifungua hizo siri saba pale ndani. Hiyo inaonyesha, inaleta mambo hayo ambayo yamefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, kusudi yafunuliwe katika siku za mwisho, kwa wana wa Mungu. Walileta Hayo sasa mbele za watu, wapate kuliona, haya, basi, kwa Huyu Bibi-arusi asiye wa kimadhehebu. Loo, jamani!

304 Hivyo hapo vitabu vyako viwili. Kimoja ni Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Jina Lako lililoandikwa Mle limechaguliwa tangu zamani Mle. Haliwezi kuondolewa, kwa sababu huwezi kamwe kuliondoa hilo hata ukifanya nini, unaona, kwa maana lilikusudiwa kuwa Mle. Lakini kwenye kile kitabu cha kawaida cha uzima, linaweza kuondolewa wakati wowote. Unaona? Usipotubu, linaondolewa, kwa vyovyote, maana utasimama Hukumuni. Bibi-arusi hata hatasimama Hukumuni; anaingia kwenye Unyakuo. Kama tu ninii . . .

305 Ninasema jambo hili, katika kufunga. Tunachelewa, kwa hiyo ni karibu saa tatu na nusu. Nasi tutakuwa tumetoka hapa ifikapo saa tatu na nusu, Bwana akipenda. Iweni na kicho sana sasa, mkasikilize. Wakati mmoja . . .

306 Ninaposema jambo hili sasa, hili linaenda kote nchini. Huko New York, sasa ni saa tano na dakika ishirini na tano. Juu kule Philadelphia na karibu kote kule, hao watakatifu wapendwa wanaoketi kule wakisikiliza, sasa hivi, katika makanisa kila mahali. Huko juu kabisa, huko chini kabisa karibu na Mexico, huko juu kabisa karibu na Canada na kila mahali, kotekote. Maili mia mbili, popote pale katika bara la Marekani ya Kaskazini hapa, karibu yote, watu wako chonjo, wakisikiliza hivi sasa. Maelfu mara maelfu, wakisikiliza.

307 Na huo ndio Ujumbe wangu kwenu, enyi Kanisa, ninyi ambao ni muungano, muungano wa kiroho kwa Neno, ya kwamba mmekufa kwa hawa waume wa kale. Mmezaliwa upya. Msijaribu kumchimbua. Yeye amekufa. Kama wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, ile chembechembe hai iliyokusudiwa tangu zamani kwa ajili yako, ni Neno likija juu ya Neno, juu ya Neno, juu ya Neno, juu ya Neno, na kufikia kimo kikamilifu cha Kristo, hiyo ni kweli, kusudi apate kuja kumchukua Bibi-arusi Wake. Sasa sisi tuko tayari tu kwa ajili ya jambo moja, hilo ni kule Kuja kwa Bwana.

308 Hilo hapo jina lako katika kile Kitabu cha Uzima. Kitabu cha Uzima ni Neno la Mungu, maana Neno ni Mungu, na Mungu ndicho kitu pekee kilicho Uzima. Kwa hiyo jina lako liliwakilishwa katika Biblia kabla Biblia haijakuwa Neno. Na kama uko hapa kufanya jambo hilo, Hilo si litathibitisha Neno hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina,"—Mh.] Kanisa si litajithibitisha Lenyewe? Si Malaiki 4, mambo haya mengine yote, kikamilifu, yatajithibitisha Yenyewe kikamilifu na kuonyesha ya kwamba Hivyo ndivyo lilivyo? ["Amina."]

309 Wakati Yesu alipokuja, Yeye alisema, "Kama nisipozitenda kazi nilizoahidiwa kwamba nitazifanya, msiniamini Mimi." Je! yeye alijiunga na kundi lipi? Alisema, "Hao wote . . . Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na kazi zake mnazifanya." Unaona? Unaona?

310 Tuko katika siku za mwisho, enyi Kanisa. Huo ndio Ujumbe wangu kwenu wa kutoa shukrani.

311 Sasa, kabla hatujafunga. Wakati mmoja nilikuwa huko juu kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mto wa Barafu. Tulikuwa tumesikia, siku nzima, ya kwamba walikuwa na—walikuwa na maporomoko, moto wa barafu ambao ungeporomoshwa usiku. Kwa hiyo watu walikuwa wakishughulika, siku nzima, wakitayarisha kitu hicho, kwa maana walikuwa wanaenda kumwaga moto huo, usiku huo. Waliweka maporomoko ya moto wa maji, kama mto mkubwa wa maji ya barafu. Lakini ni . . . Ilionekana kama upinde wa mvua, karibu hivyo, unapotokea, wa moto huo ukiporomoka kutoka kwenye mto huu wa barafu. Kila mahali kwenye hifadhi hiyo, mimi na mke wangu, na watoto, tulitembea siku nzima. Tulitaka kukaa, tupate kuona maonyesho hayo ya moto. Kwa hiyo tu—tu—tuliahidiwa

ya kwamba tungeuona, na tungeushuhudia tena. Walisema yanaendelea katika msimu wote wa kiangazi na kadhalika. Nikasema, "Vema, tutaweza kuuona?"

312 Walisema, "Tuliahidi jambo hilo usiku wa leo. Tumeahidiwa jambo hilo." Kasema, "Wako huko juu wakiutayarisha."

313 Baada ya yote kutayarishwa kwa ajili ya tukio hilo! Hilo ndilo linalotendeka sasa hivi. Yote yanatayarishwa kwa ajili ya lile tukio, Kanisa likivutwa litoke kwa ajili ya Jina Lake, kumchukua Bibi-arusi Wake atoke miongoni mwa ulimwengu, madhehebu haya na ulimwengu mzima, na uchafu na mambo ya ulimwengu.

314 Kila mtu; hilo tukio lilitayarishwa. Kila mtu alikuwa amesimama nje. Wakasema, "Sasa endeleeni kuangalia, moja kwa moja kule juu ya mlima."

315 Hivyo ndivyo limekuja daima. Hivyo ndivyo litakavyokuja wakati huu. Hivyo ndivyo linavyokuja daima. Si kupitia kwa dhehebu fulani! Kamwe Mungu hajatumia madhehebu, hata!

316 Mtengenezaji anajitokeza, analichukua Neno la Bwana. Ndipo wakati akifa, wanaunda dhehebu kutoka kwake. Hivyo ndivyo Wapentekoste na wengine wote walivyofanya. Wakati hoja mpya zinapotokea na kila kitu, hivyo ndivyo ilivyo. Hivyo ndivyo jambo hilo lilivyotokea. Neno jipya linaongezwa, ndipo wanajenga kanisa kutoka kwake, wanaunda madhehebu, wakajitenga. Ilibidi iwe hivyo.

317 Sasa, huwezi kushinda—huwezi kuyashinda maumbile. Maumbile hufuata utaratibu ule ule, sikuzote: shina, jani, kishada, kadhalika, kapi, halafu ngano.

318 Sasa angalia. Yote yalikuwa tayari. Kila kitu kilikuwa kimewashwa moto na kufanywa tayari. Na kila mtu alikuwa amesimama nje. Nilikuwa nimeinua kichwa changu; mkono wangu umemkumbatia mke wangu. Tulikuwa tukiangalia. Na watoto wamesimama pale, sisi sote tukiangalia juu, namna hiyo. Jamani! Ilikuwa ni ajabu sana, maana tulikuwa tukiutarajia. Tulikuwa tumeahidiwa.

319 Amina! Neno linaahidi jambo Hili. "Itakuwa, kabla haijaja ile siku iliyo kuu na ya kuogofya ya Bwana, tazama, nitawapelekea Eliya nabii. Ataigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao." . . .?. . . "Itakuwa katika siku za mwisho, nitaimwaga Roho Yangu kutoka Juu." "Mvua ya vuli na ya masika zitamiminika kwa pamoja katika siku ya mwisho." Ahadi zote hizi, kote katika Maandiko, zimetolewa. Tunaangalia juu. Mtazame Bibi-arusi wa kweli kote nchini wakati huu, akiangalia juu. Enyi Kanisa, Yeye yuaja, moja ya siku hizi. Kwa uhakika tu kama alivyokuja ile mara ya kwanza, Yeye yuaja tena. Wekeni tayari kila kitu. Jitengeni na kapi. Tulieni mbele za Mwana. Endeleeni kuangalia juu. Iweni katika matarajio.

320 Mara, tulisikia kitu fulani kutoka juu ya kile kilima, sauti ilishuka kupitia kwenye kipaza sauti, ikasema, "Mambo yote yako tayari."

321 Halafu mtu huyu, akisimama pale pale karibu na mimi, akasema, "Moto na ushuke." Huu hapa waja, ukitiririka kote kwenye ule mlima, moto wa mto wa barafu na ndimi za moto zikiramba, tamasha la ajabu.

322 Ndugu, hebu na tutayarishe mambo yote, kwa kuwa moja ya siku hizi Moto utashuka. Tunapaa juu. Sasa hebu na tujitayarishe kwa ajili ya wakati wa kushuka kwa Moto. Tuko katika siku za mwisho, sote tunajua jambo hilo, na tuko tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana. Jambo la kufanya ni kujitenga na dhambi zote. Jitenge na chochote kinachohusu ulimwengu. "Usiipende dunia wala mambo yaliyomo duniani."

323 "Usiache mtu yeyote, kwa kanuni yake ya imani, akudanganye." Wewe dumu moja kwa moja katika ahadi ya Mungu, Neno la Mungu. Na Neno hilo, kama ni Neno la siku hii, Mungu analithibitisha kwamba ndivyo lilivyo. Asipolithibitisha, hilo si Neno la siku hizi.

324 Neno lililoshuka katika Siku ya Pentekoste halitafaa leo. La, bwana. Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya Pentekoste. Hili ni la Bibi-arusi, kwenda Nyumbani kwa Bibi-arusi. Tuna kitu tofauti. Wapentekoste waliwakilisha jambo hilo, tena. Tuko katika wakati wa Bibi-arusi. Si zaidi ya vile Ne—Neno la Nuhu lingefaa katika siku za Musa; si zaidi ya vile torati ya Musa ingeweza kufanya kazi katika wakati wa Paulo hapa. Yeye alijaribu kuwaambia, "Mmekufa kwa jambo hilo, wala hamwezi kuchukua jambo hilo."

325 Enyi Kanisa, ninyi ambao ninawazungumzia, usiku wa leo, kote nchini, kama—kama mmejitenga na madhehebu na uchafu wote na mambo ya ulimwengu huu, na mambo yote hayo yanayowaweka katika kanuni za kujibunia na desturi na mambo kama hayo, ulijitenga: Angalia juu. Iweni tayari. Moto utashuka, moja ya siku hizi. Mungu atamwacha Yeye aje, na ni tamasha la ajabu. Je! utakuwa tayari wakati atakapokuja? Je! utakuwa tayari kupaa juu pamoja Naye wakati atakapokuja? Kunyakuliwa kwa siri kwa Bibi-arusi wa kimbinguni, "Atafanywa afa. . .kutoka afaye kuwa asiyekufa; atabadilishwa, katika dakika moja, kufumba na kufumbua. Sisi tulio hai na tuliosalia hatutawatangulia hao waliokwisha kulala mauti."

326 Hivi majuzi, kwenye Siku ya Kukomesha Vita, nilikuwa nimesimama huko chini Tucson. Mvulana wangu mdogo alitaka kuona gwaride. Nilikuwa nikisoma, wala sikuwa na wakati wa kufanya hivyo. Na nilikuwa nimepokea simu nyingi sana za wagonjwa na kadhalika. Kwa hiyo akasema, "Baba, wamekataa kunipeleka." Akasema, "Nipeleke."

327 Nikasema, “Vema.” Ndugu Simpson, nafikiri yuko hapa; na mvulana wake mdogo alitaka kwenda. Kwa hiyo nikawaingiza haraka kwenye gari tukateremka haraka huko.

328 Nilisimama pale pembeni na kuangalia. Na baada ya kitambo kidogo, nikasikia, huko nyuma mbali sana, mdundo unakuja, “ndu, ndu,” ngoma, zikipigwa. Nilisimama pale. Nikawazia, “Vema, maskini watoto hawa, kweli wanasoma vitabu hivi vyote juu ya jeshi. Kweli watapenda jambo hilo.” Nikaona, hiki hapa kifaru cha kale cha Vita vya I vya Dunia kinatangulia. Hivyo hapo vinakuja, vitu vidogo kama hivyo. Kilichofuata, baada ya hivyo; kilichokuwa kinafuata hivyo kilikuwa ni kile kifaru kikubwa kipya cha Sherman cha Vita vya Pili vya Dunia, chenye kizibo cha mtutu juu yake. Ndipo kingine kikafuata, na kingine, baada ya kitambo kidogo wakaja Mama wenye Nyota ya Dhahabu.

329 Halafu basi, baada ya kitambo kidogo, wakaja mashujaa kumi na wawili wa vita waliosalia, katika mkoa mzima wa Arizona, kutoka katika Vita vya Kwanza vya Dunia; mashujaa kumi na wawili wa vita. Baada ya hao, kukaja mkokoteni, askari asiyejulikana, msalaba mdogo mweupe. Huyo hapo baharia amesimama, mwanamaji, na askari, analinda zamu; kulikuwa na chumba kidogo kwenye ule mkokoteni. Upande wa pili kulikuwako na maskini mama mzee mwenye mvi, ameketi huku amebandikwa nyota ndogo ya dhahabu kwa pini, maskini mke wa kupendeza akilia, mumewe amekufa; maskini mvulana mdogo aliyevaa matambara, amegeuza kichwa chake. Baba yake aliuawa. Na halafu nyuma ya hao kukaja wengine zaidi na zaidi na zaidi, ndipo likaja jeshi jipya. Nilisimama pale. Ni tamasha la ajabu jinsi gani, bali ni huzuni jinsi gani!

330 Nikawaza, “Ee Mungu, moja ya siku hizi nitashuhudia tamasha jingine.”

331 Kutakuwako na siku ya ufufuo, ambayo, “Wa kwanza watakuwa wa mwisho; walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.” Manabii wa kale watatokea, kwanza, nao wataona maandamano hayo yakienda, yakitembea kuelekea juu hewani. “Ndipo sisi tulio hai na tuliosalia hatutawazuia hao waliokwisha kulala mauti. Kwa kuwa baragumu ya Mungu italia, wafu katika Kristo watafufuliwa kwanza.” Tutaingia moja kwa moja mstarini pamoja na hao watakaoingia, haleluya, wote huko nyuma kote katika wakati wa Luther, Wesley, Methodisti, Presbiteri, na kuendelea hata kufikia wakati wa mwisho, ambao walilipokea Neno katika wakati wao.

Mungu awabariki. Wekeni mambo yote tayari, na huo Moto utashuka.

332 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Sijui, katika wasikilizaji hawa wanaoonekana usiku wa leo, wakati nimewashikilia hapa kwa. . .mpaka saa tatu na nusu. Kuna

mmoja hapa, kuna dazani moja hapa, ni wangapi hapa, nao wanasema, "Ndugu Branham, ninajionea aibu, jinsi nilivyoishi. Nimeshughulikia madhehebu na wanadamu sana. Ninajua ya kwamba siko sawa na Neno la Mungu. Nitakuomba tu uniombee, Ndugu Branham"? Inua mkono wako. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Angalieni tu, huko juu kabisa kwenye roshani, kila mahali. Mungu awabariki. "Ninajua. . . " Sasa msione aibu. Sasa, msione aibu.

333 Na huko nje, kote nchini, kutoka New York mpaka California, kutoka Canada hadi Mexico: ninyi watu ambao mmekusanyika katika makanisa (hayo ambako hayo makundi madogo manyofu ambayo yameamini Ujumbe huu kwa mioyo yao yote; wametoka, wametoka katika dhiki kuu, wametoka kupitia madhehebu hayo; wao ni vito vya Uzima) Je! unasikia shauku, usiku wa leo, kama maskini yule tai mdogo, kwamba unasikia kitu Fulani ambacho ni tofauti kidogo na yale uliyosikia, lakini, hata hivyo, moyoni mwako unajua ni Kweli? Wewe, kule ndani, kuna mchungaji anayesimama pale mahali fulani. Umeinua mkono wako. Nitakuombea.

334 Mambo haya hayakufanywa kisiri, ewe rafiki. Kumbuka, "Mlango ni mwembamba na njia imesonga, na ni wachache watakaoiona." Usiambatane na umati huo wa watu unaoenda ng'ambo ile, ewe rafiki, huo Wakati wa Kanisa la Laodikia. Wangeweza kurukaruka, wacheze kwa muziki, vuguvugu. Halikusema walikuwa baridi kama barafu sasa. Lilisema, "Walikuwa vuguvugu," hao ni Wapentekoste, "wala hawajui ya kwamba ni wenye mashaka, wanyonge, vipofu." Vipofu kwa kitu gani? Neno, kwa udhihirisho wa Neno; kwa maana halikupitia kwenye madhehebu yao, hawawezi kulipokea.

335 Nanyi wahudumu kule chini Tucson, usiku wa leo, siwawajibishi kwa jambo hilo. Mungu ndiye anayewawajibisha. Nilikuwa huko kwa muda wa miaka mitatu. Niliwaambia nisingeanzisha kanisa. Sikulianzisha. Ndugu Pearry Green alilianzisha. Nilikuwa huko kwa muda wa miaka mitatu, wala hakuna hata wakati mmoja mlinialika kwenye mimbara yenu. Nilikaa Tucson kwa karibu miaka mitatu. Mungu atanitoa jangwani moja ya siku hizi. Ujumbe huu hauna budi kudumu. Nilijaribu nilivyoweza kuingia kwenu. Ni— ninajua sababu hamkunialika. Mnasikia? Sababu tu ya ninyi kutonialika, madhehebu yenu yangewafukuza. Nanyi mnajua, nimezungumza na wengi wenu, kule kwenye Mkahawa wa Furr, nanyi mnajua hiyo ni kweli. Oneni aibu.

336 Tokeni kwake. Toka humo, ndugu. Kama kuna Uzima wowote ndani yako, utakuwa kama maskini yule tai mdogo ambaye ndio kwanza ninene habari zake, utasikia Neno la Mungu. Kumbuka, utalisikia Hili kwa mara ya mwisho, moja ya siku hizi. Tuko karibu sana sasa. Mbona usije, usiku wa leo?

337 Mungu mpendwa, tumeketi kwa kicho sasa, kweli hii ni siku ya kutoa shukrani, Bwana. Ninashukuru, Bwana, kwamba ninaishi katika siku hii. Hii ndiyo siku iliyo kuu sana. Mtume Paulo alitamani kuiona siku hii. Wale watu mashuhuri wa zamani walitamani kuiona. Manabii walitamani kuiona. Waliitazamia siku hii. Ibrahimu aliitazamia siku hii, kwa kuwa aliutafuta Mji ambao Mwenye Kuujenga na Mwenye Kuubuni alikuwa ni Mungu; unaning'inia moja kwa moja juu yetu, usiku wa leo. Yohana aliona Roho wa Mungu akishuka kutoka Mbinguni, alishuhudia, alijua ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Na, wazia sasa, Yeye anamchagua Bibi-arusi Wake.

338 Mungu mpendwa, kote huko nje nchini, nena na moyo wao. Wewe ndiwe tu unayeweza kuubadilisha moyo wao. Kama hiyo haikuwa ni Mbegu iliyowekwa humo ndani hapo mwanzo, kamwe hawataliona, Bwana. Wao ni ninii tu… "Kipofu atamwongoza kipofu mwenziwe. Wataanguka shimoni," hakika kabisa, kwa kuwa Neno Lako linasema wataanguka.

339 Sasa, Baba, kwa kuwa tunaona kote nchini, kote ulimwenguni, katika Afrika, idadi kubwa, idadi kubwa kupitia Afrika Kusini, Msumbiji, kote nchini, makusanyiko madogo yakichukua kanda hizi. Na kwa hiyo hii kanda itaenda kwa mataifa ishirini na kitu, mataifa mbalimbali. Wanaanza kuliona na kujiondosha, mamia na mamia yao. Hutachukua wengi, Bwana. Ndipo hapo yule mshiriki wa mwisho atakapopokelewa kwenye ule Mwili, Kristo atakuja.

340 Bwana Mungu, ninamwomba Bibi-arusi, usiku wa leo, yule ambaye nimeona amejiondoa na anangojea, jalia wajitenge na kila kitu kilichoko ulimwenguni. Hawana budi kukaa katika Uwepo wa joto la Nuru ya Mwana wa Mungu, wakioga katika Neno Lake, katika upendo Wake. Tujalie hayo, Mungu mpenzi.

341 Jalia watu hawa hapa, wanaoonekana, walioinua mkono wao, usiku wa leo, madazeni yao kote katika maskani hii kuu. Ninaomba, Mungu, ya kwamba Uzima mpya utaingia ndani yao; ninaomba jambo hilo, kwa ajili ya kote nchini na hata kote ulimwenguni, ambako kanda hii itachezwa, ya kwamba wao pia watapokea Ujumbe huu wa kutoa shukrani na wajue, kwa madokezo na mambo kadha wa kadha ambayo yametupwa, kile wanachopaswa kufanya. Ninaomba hayo, Baba. Tujalie. Wabariki. Hao ni Wako.

342 Ninajua ni kawaida sasa, Baba, ya kwamba tunawaomba watu waje madhabahuni. Na ninaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba katika kila misheni, kila mahali huku, na kote ulimwenguni, ya kwamba watakuja madhabahuni; watu weusi, wazungu, manjano, hudhurungi, popote walipo; matajiri, maskini, wasiojali, ombaomba, wowote wale.

343 Watu wa kimadhehebu, hao walioketi wenye ubinafsi na wenye kujipenda mno, Ee Mungu, "Uchi, wenye mashaka, wanyonge, vipofu, na hata hawajui." Ulisema ingekuwa namna hiyo, na ndivyo ilivyo.

344 Hivyo ninaomba, Baba, ya kwamba utaita kila Mbegu, usiku wa leo. Na kila mahali kote ulimwenguni ambako huenda Huu ukaangukia, naomba umshike maskini yule tai mdogo anayeijua Sauti ya Bwana Wake. Tujalie hilo, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu. Amina.

345 Sasa huku vichwa vyenu vimeinamishwa, hapa katika kusanyiko hili linaloonekana. Hivi baadhi hapa, ambao hamjaokoka, hata hamjampa Mungu moyo wenu, hivi hamdhani mnapaswa kutoa shukrani kwa ajili ya yale Yesu aliyowafanyia? Kuwazia, ya kwamba wewe ni mwenye dhambi, ya kwamba umetenganishwa na Mungu, na hata hivyo kitu Fulani moyoni mwako, kinapiga hodi. [Ndugu Branham anagonga mimbarani—Mh.] Unajuaje kama wewe si mmoja wa maskini hao tai wadogo! Una mashaka, na utakuwa na mashaka, mpaka utakapojisalimisha Kwake. Mbona usiifanye hii moja ya kutoa shukrani iliyo kuu sana uliyopata kuwa nayo, hapo ulipompokea Yesu Kristo kama Mwokozi Wako.

346 Unaweza kuja hapa na kusimama madhabahuni? Nitaomba pamoja nawe kama utakuja, mwenye dhambi yeyote, mwanamume ama mwanamke, mvulana ama msichana, uwe ni mfuasi wa kanisa ama si mfuasi wa kanisa. Kuwa mfuasi wa kanisa hakukufanyi Mkristo sasa. Madhabahu iko wazi. Je! utakuja, mwenye dhambi yeyote ambaye angetaka kuja, kumpokea Bwana Yesu Kristo. Ungetaka kweli kuacha . . .

347 Baadhi yenu ninyi wa madhehebu ambao mngetaka kuacha kula chakula hicho cha kuku, cha kusema, "Wewe ni mfuasi wa *hili* na ni sawa." Je, unataka kweli kujua ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu ni nini? Njoo, uone.

348 Madhabahu iko wazi. Tuko tayari. Njoo tu huku moja kwa moja, kutoka—kutoka kwenye kiti chako. Njoo moja kwa moja na upige magoti hapa madhabahuni, ndugu huyu ambaye ndiyo kwanza aje.

349 "Kutoa shukrani, Ee Mungu, ninakushukuru sana. Kwamba, maishani mwangu mwote, nimejua kumekuwako na jambo fulani, Bwana. Kamwe sijatosheka. Nimejaribu. Ni—nilifikiri, 'Mwaka ujao, nitafanya hivyo. Juma lijalo, nitafanya hivyo, nitakaposikia tena wito wa madhabahuni. Nitafanya hivyo, siku moja.' Ninaliahirisha, na kuliahirisha. Lakini, Bwana, ninajua nina kasoro. Daima nitaamini ya kwamba kulikuwa na jambo fulani tofauti. Na sasa, Bwana, usiku wa leo, ninashukuru kwa ajili ya matayarisho yaliyofanywa na Mwana wa Mungu, kwamba dhambi zangu, kwa kweli kutokuamini kwangu, kungesafishwa kuondolewe kutoka kwangu. Ninakuja, usiku

wa leo, na kupiga magoti kukubali zile baraka kuu za kutoa shukrani ambazo Yesu Kristo alizitoa kwangu aliponifia pale Kalvari."

350 Je! utakuja? Sasa kuna watu wanaopiga magoti hapa madhabahuni. Mbona usiamke na uje? Umetaka kufanya jambo hilo. Umejaribu.

351 Wazia tu juu ya Ndugu Lyle Palmer, ndugu yetu mzuri, wa thamani. Alikuwa ameketi uwanjani, ndivyo ninavyofahamu, akimwangalia msichana wake mdogo akicheza krokei huko nje, ama kitu kama hicho, naye akaanguka kitini na alikuwa amekufa kabla hata hajaweza kusogea. Hujui ni wakati gani utakapoondoka hapa. Hujui kamwe ni wakati gani ambao utaondoka. Huenda ikawa bado, ni usiku wa leo, kwa hiyo mbona usije na kumalizana na jambo hilo sasa?

352 Njoni, enyi watu. Hivi hamwezi kuhisi kitu Fulani kikiwavuta? Ni—ninajua kuna wengi wenu hapa ambao wanapaswa kuwa papa hapa madhabahuni, na watu hawa sita ama saba sio tu wanaoketi humu ndani. Sasa, kama mnaniamini mimi na kuangalia hapa mimbarani, mambo yanayotendeka, niaminini sasa. Siku moja sauti yangu itanyamazishwa. Hamtaisikia tena. Ungalitamani ungalikuja.

353 Mnasema, "Lakini, Ndugu Branham, nimekuwa mfuasi wa kanisa." Hilo halileti tofauti yoyote kile umekuwa. Vivyo hivyo—vivyo hivyo Nikodemo naye alikuwa ni mfuasi wa kanisa. Vivyo hivyo na Yohana, Petro, Yakobo, Paulo, hao wengine wote walikuwa ni wafuasi wa kanisa.

354 Paulo alikuwa ni mfuasi wa kanisa mpaka jambo fulani likatukia usiku mmoja, ama ilikuwa ni siku moja, naye akaja. Alikuwa ni mfuasi wa kanisa aliyebadilika basi, akawa mwana wa Mungu. Je! hutakuja? Loo, alikuwa amepewa mafunzo. Alikuwa ni msomi. Alijua alikuwa amepewa mafunzo, moja ya shule kuu sana za kutoa mafunzo zilizokuwako, Gamalieli, mmoja wa waalimu bora sana waliokuwako nchini. Lakini alijua alihitaji kitu fulani.

355 Mbona usije? Mara nyingine tena ninawaomba. Katika mahali ambapo . . . Hapa ama kote nchini, ninawaomba, popote mlipo, katika kusanyiko lolote mlimo, kwenye saa hii ya kutoa shukrani. Kumbukeni, ninarekodiwa kwenye kanda hapa; si hapa tu, bali Mbinguni pia.

356 Unajua, imethibitishwa kisayansi ya kwamba kila hatua unayopiga inarekodiwa. Wamethibitisha jambo hilo. Kumbukeni, televisheni ilithibitisha jambo hilo. Televisheni hai—haitengenezi picha. Wewe ndiwe picha. Yenyewe inatuma tu yale unayofanya, ikayaingiza kwenye mtandao fulani. Wewe uko hapo, hata hivyo. Unaona? Unaposogeza kidole chako, msogeo huo huzunguka kote ulimwenguni. Kila wakati unapovaa rinda, sura yako inaenda kote ulimwenguni. Imerekodiwa. Kila wazo

linalopitia akilini mwako liko kwenye rekodi. Na siku moja rekodi hiyo itaacha kucheza, itawekwa kwenye albamu.

357 Ndipo kwenye ile Hukumu itarudi tena. Wewe upo hapo umesimama na nywele zilizokatwa, ukidai wewe kuwa ni Mkristo. Wewe upo hapo umesimama na mawazo akilini mwako dhidi ya Neno, na yako moja kwa moja kwenye akili yako. Huwezi kuficha jambo hilo. Kumbuka, televisheni, sayansi hata inajua jambo hilo ni kweli. Uko sasa hivi umesimama, ukijua ya kwamba unapaswa kuwa hapa, kumbuka, wakati haya yanaporekodiwa, kwenye hiyo Siku ya Hukumu, wazo lilo hilo ulilo nalo sasa litarudi moja kwa moja kupita kwenye akili yako tena. Hilo litakuwa moja kwa moja kwenye rekodi. Ulimwengu mzima utaliona likichezwa. Mbona ulimwengu haunínii... Wakikuangalia, kwenye Siku hiyo ya Hukumu, Malaika wote wakiwa hapo.

358 "Kama ukinionea aibu Mimi hapa, wakati picha yako inapopigwa sasa, kwenye Siku ya Hukumu nitakuonea aibu. Kwa maana, Mimi nililitia mafuta Neno Langu, nikakutumia Hilo. Usingeliamini. Ulijificha nyuma ya kitu fulani."

359 "Loo," unasema, "mimi ni mwema vya kutosha. Nimefanya *hili*. Nimecheza katika Roho. Nimenena kwa lugha." Kafiri naye hufanya vivyo hivyo. "Nilipaaza sauti." Kafiri naye hufanya vivyo hivyo. Unawezaje kulipa Neno kisogo basi?

Kwa nini?
Kwa nini usije Kwake sasa?
Kwa nini? Kwa nini?
Kwa nini usije Kwake sasa?

Mbona unakawia, ndugu mpendwa?
Loo, mbona unakawia muda mrefu sana?
Yesu anangoja apate kukuwekea
Mahali katika Nyumba Yake iliyotakaswa.

Akuweke uwe mmoja wa washiriki wa Mwili Wake!

Kwa nini usininii?

Loo, maskini tai mdogo, njoo sasa.

Loo, mbona usije?

360 Bwana ninashukuru. Ninashukuru sana. Nikikushukuru Wewe, Bwana; si kwa ajili ya chakula cha kawaida, ingawa na kwa hicho pia. Lakini, Bwana, wakati wa mwisho umewadia. Ninashukuru kwa ajili ya Chakula hiki cha kiroho, Bwana, Chakula cha kiroho cha Mihuri Saba iliyoahidiwa kufunguliwa.

Unasema, "Hiyo itakuwa ni kitu cha tofauti." La, la.

361 Huwezi ukaongeza Neno moja. Na kuchukua...Imo Mle ndani tayari, ni kwamba tu imefichwa. Imefungwa. Ni wangapi wanafahamu jambo hilo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona?

Mnasema, "Vema, hiyo siri itatokea." Loo, la.

362 Imekwishaandikwa tayari. Huwezi kuongeza Neno moja Kwake, wala kuondoa moja Kwake. Unaona? Imo Mle ndani tayari. Inabidi tu ifunguliwe katika siku ya mwisho.

363 Mbona usije? Njoo sasa, ewe rafiki. Kama huwezi kufahamu, njoo. Piga magoti, zungumza Naye juu ya jambo Hilo. Kama siwezi kulifanya dhahiri kwako, Yeye atalifanya, kwa kuwa Yeye ni—ni Mwondoa mashaka yote.

. . . katika kiti Chake cha enzi kitakatifu.

Loo, kwa nini usije? Kwa nini usije?
Kwa nini usije Kwake sasa?

364 Kumbuka, huu unarekodiwa, si katika kanda hii peke yake, bali katika rekodi kubwa ya Mungu. Kila mmoja wenu, kila hatua, unapoinamisha kichwa chako, unapoinamisha moyo wako, wazo linalopitia akilini mwako, kumbuka, linarekodiwa hivi sasa Utukufuni, na rekodi hiyo itachezwa katika Siku ya Hukumu. U wapi uamuzi wako? Loo, jinsi utakavyotamani ubadilishwe, kwenye Siku hiyo.

365 Nitasubiri tu, kwa kuwa wapo wengi, wengi sana wamezunguka madhabahu sasa. Mnaona? Labda mmoja wao, kama tu ningalisubiri kidogo zaidi, huenda kukawa na mwingine huko nje, huenda ikawa yuko mahali fulani huko New York, heunda ikawa ni mahali fulani huko Philadelphia, huko California, Arizona. Mahali fulani, huenda ikawa kuna mwingine anayekuja. Mchungaji, popote ulipo, usiache wito wa madhabahuni sasa.

366 Huenda tusione Kutoa Shukrani kwingine. Huku kunaweza kukawa ndiko kwa mwisho, na rekodi zitachukuliwa ziwekwe, usiku wa leo, kwa mara ya mwisho. Kanda itakwisha, moja ya siku hizi. Rekodi itaondolewa na itakuwa iko kwenye albamu ya Mungu. Ndipo itachezwa tena, vile mawazo yako yalivyo sasa. Usije ukasema hukujua vinginevyo. Unajua. "Bali hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watanijia."

. . . njoo Kwake?

367 Ninaamini, kama ningekuwa nimeketi pale nje mahali fulani, na ningekuwa na wazo lililo dogo sana, ningekimbilia hapa upesi niwezavyo. Naam.

Loo, mbona usifanye hivyo? Kwa nini?

368 Je! umefikia uamuzi wa mwisho? Je! una hakika humhuzunishi Roho Wake sasa? Hebu na tuendelee kuinamisha vichwa vyetu basi. Je! una hakika hujamhuzunisha Roho Wake? Una hakika umefanya vile hasa alivyokwambia ufanye? Una hakika sasa? Kumbuka, hu—huenda kamwe usipate nafasi nyingine. Hiyo rekodi inaweza ikakamilika, usiku wa leo. Hii huenda ikawa ndiyo ya mwisho kabisa. Huenda ikawa hii ndiyo

kanda ya mwisho kwa ajili yako. Je! una hakika uko tayari sasa? Kama uko tayari, naliacha hilo mikononi mwako, katika Jina la Bwana Yesu.

369 Sasa wakati kwaya ikiimba polepole, nitawaombea hawa walio hapa chini. Kwa namna fulani mimi ni Mkristo wa kipekee sana. Ninaamini ya kwamba Mungu ndiye wa kuokoa. Ninaamini ya kwamba Mungu hana budi kulipanda Neno. "Mimi Bwana," yasema Biblia, Isaya, "Mimi Bwana nimeipanda. Nitaimwagilia maji, usiku na mchana, asije mtu akaipokonya kutoka mkononi Mwangu." Kabla sijamwomba mtu yeyote kuja hapa madhabahuni pamoja na watu hawa, ninataka kuwaombea, mimi mwenyewe.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

370 Yesu mpendwa, ndiyo kwanza nilinukuu tu Neno Lako, ambalo nabii Wako alisema, nami ninajua maneno ya manabii ni kweli. Nawe ulisema, "Mimi Bwana nimelipanda." Mbona, hakika, ulililiweka kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Mimi Bwana nimelipanda, Nami nitalimwagilia maji, usiku na mchana, asije mtu akalinyakua kutoka mkononi Mwangu." Hawa, labda, Bwana, wamesikia miito mingi ya madhabahuni. Bali ungali unalimwagilia maji, Bwana.

371 Hawa hapa, usiku wa leo. Naomba tu waachilie, usiku wa leo, Baba, mambo yote ya ulimwengu, dhambi zote na matatizo yaliyo moyoni mwao, na kwa akili zao timamu tu, kwa kicho, moyoni mwao, wajisalimishe kwa Neno Lako, sasa hivi, waseme, "Bwana Yesu, ndani ya moyo wangu, daima nimeamini ya kwamba kulikuwa na kitu fulani kwa ajili yangu, ambacho kamwe sijakipokea bado. Ingawa nimejaribu, kama vile hayo maneno yalivyonenwa usiku wa leo, kumfuata yule kuku, bali kulikuwako na kitu fulani kilichoonekana ni kigeni kwangu. Hakikusikika kiko sawa kabisa. Basi, usiku wa leo, ninajisikia ya kwamba ninakaribia zaidi kuingia katika mikono ya Neno lililo hai. Ninakuja hapa kwa kicho vivyo hivyo, nikiwa na akili timamu. Nimeketi hapa chini karibu na madhabahu hii. Ninataka wokovu, Bwana, sana. Nina njaa sana! Ninakutaka wewe, Bwana, unishike mikononi Mwako, usiku wa leo. Si kwa mhemuko wowote, bali kwa Roho wa upendo, nichukue mikononi Mwako, Mungu mpendwa."

372 "Mimi ni mtoto Wako. Ninajisikia ya kwamba mimi ndiye yule tai waliyekuwa wakinena habari zake. Nidake, Bwana. Ninaruka. Nimesimama kutoka kwenye kiti changu, na kupiga magoti hapa chini. Nidake, Bwana. Ninaruka. Nilete kwenye Mbawa Zako, Bwana, mbali na mambo haya ya ulimwengu. Jalia niruke kutoka kwenye uchafu wa ulimwengu huu, kutoka kwenye tabia yangu mbaya, kutoka kwenye mapokeo yangu yote ya kimadhehebu. Jalia nije Kwako tu, Mungu mpenzi, ili

kwamba Roho Mtakatifu Wako apate kunimwagia msamaha wa mashaka yangu yote. Nijalie mimi, usiku wa leo, nifanyike mtoto Wako, mpya, aliyezaliwa, na kiumbe kipya, usiku wa leo. Nidake. Nibebe, unipeleke mbali na kilio cha kuku. Nibebe, unipeleke kwenye kiota cha Tai, ambamo humo ningeweza kulishwa kwa Neno la Mungu, mpaka nitakapoweza kuruka."

373 Tujalie hilo, Mungu mpenzi. Wachukue. Hao ni Wako. Haya ndiyo maombi yangu kwa unyofu, nikiwaombea watu wanaokufa. Tujalie hilo, Baba. Ninaomba ombi hili kwa niaba yao. Kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ninaomba.

Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu.

374 Sijui, hapa madhabahuni sasa, ni ninyi mliopiga magoti hapa. Wengi wenu mmedai kuwa ni Wakristo, bali mmejisikia ya kwamba kuna kitu fulani daima, mahali fulani, ambacho hamkuwa nacho. Huenda umekwishafanya matendo yote ya kidini. Huenda umepiga makelele. Huenda umefanya mambo yote. Huenda umecheza katika Roho. Huenda umenena kwa lugha. Wala hakuna mtu anayeweza kusema jambo lolote baya dhidi yake. Hiyo ni kweli. Hayo yote ni mema. Lakini, unaona, hizo ni *karama* za Roho, bila ya Roho. Kama Roho angalikuwako, kusingekuwako na huko kujisikia kuhukumiwa namna hiyo.

375 Hivi kwa kweli ninyi, kwa unyofu, hapa madhabahuni, mnaamini kwamba sasa hivi, wakati mkiwa hapa, ya kwamba tendo tu la kujisalimisha, si mhemuko sasa, bali kwa imani halisi, isiyoghoshiwa, ya kwamba Mungu atawapokea na kuwalea kwa Neno Lake mpaka mmekuwa tai, ninyi wenyewe, na mnaweza kuruka? Kama unaamini, na unataka Mungu afanye jambo hilo, inua mkono wako, ninyi mnaozunguka madhabahu hapa chini. Mungu awabariki. Kila mmoja ameinua mikono yao juu.

376 Sasa, kwa unyenyekevu sana, nitawaomba wanaume na wanawake waliowekwa wakfu ambao wanamjua Mungu kweli.

377 Karibu wote, ni ajabu sana, inaonekana kana kwamba ndivyo ilivyo, miito ya madhabahuni ninayofanya huwa karibu yote ni wanaume. Mnajua, kwa kawaida, ni wanawake. Bali wote hapa ni wanaume. Nafikiri kuna mwanamke mmoja madhabahuni, usiku wa leo, labda wawili. Kwa kawaida huwa ni wanawake. Lakini, kwa njia moja ama nyingine, nadhani inaonekana kana kwamba wanawake wanafikiri ya kwamba mimi ninawachukia. Siwachukii, dada. Watatu, ninaamini, mtu fulani alisema wanaona. Siwezi kuona juu ya madhabahu hapa. Vema.

378 Baadhi yenu ninyi Wakristo mliowekwa wakfu njoni hapa mkasimame pamoja nami katika maombi kwa dakika moja tu. Madhabahuni, popote mlipo, jukwaani, mtu fulani anayemjua Mungu kwelikweli, anayejua tu jinsi ya kusimama hapa kwa dakika chache tuombe pamoja nao, ndipo tutawaruhusu

wasikilizaji wafumukane. Kila mtu na awe na kicho sana sasa. Msiondoke. Njoni tu hapa na msimame hapa.

379 Baadhi yenu ninyi watu ambao kweli mnaamini Hili kwamba ni Kweli, ya kwamba tunaingia katika wakati mwingine. Tunaingia katika Wakati wa Kunyakuliwa. Mnajua kanisa haliwezi kwenda katika hali yake, wala haliwezi kuwa bora zaidi. Halina budi kuharibika zaidi. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Halina budi kuwa baya zaidi. Wala haliwezi kwenda namna hii. Unaona? Inabidi jambo Fulani litokee, na linatendeka sasa hivi, rafiki. Li—li—linaendelea, uamsho unaendelea kwa ajili ya Bibi-arusi. Hiyo ni kweli. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

380 Njoni huku sasa, ninyi Wakristo mliowekwa wakfu mnaotaka rekodi ye—yenu kuona jambo hilo, hawa wanaokuja kwa uaminifu, mnaotaka kuja na kuomba pamoja nao, kama ndugu zenu na dada zenu, njoni hapa madhabahuni. Simameni hapa karibu kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi. Kuna mtu mwingine anayetaka kuja, kusimama hapa? Piga tu magoti karibu nao. Tembeeni tu, ambapo ninyi wanaume mtakuwa nyuma ya hao wanaume; ninyi wanawake. Waombeeni kwa upendo, unyenyekevu.

Mungu mpenzi, saidia . . .? . . .

381 "Ninatoa yote. Ninatoa dhehebu langu. Ninavunja arusi yangu ya kwanza. Ninaachana na mume wangu wa kwanza. Ninatoa yote, Bwana."

> . . .-misha yote.
> Yote Kwako, Ee Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Ninatoa yote.
>
> Ninatoa yote,
> Ninato-. . .

382 Je! unaachana na wazo lako mwenyewe? Je! unaweza kuachana na mawazo yako mwenyewe, kwa Neno la Mungu?

> Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
> Ninatoa yote.
>
> Ninatoa yote,
> Ninatoa yote.
> Yote Kwako, Ee Mwokozi mbarikiwa,
> Natoa.

383 Wote wanaoamini sasa, katika kusanyiko hili, simameni. Hebu na tuuimbe, pamoja, sasa.

> Ninato-. . .

Nyote mmejitolea, mko tayari kuuimba sasa?

> Ni-. . .
> Kwako, Ee Mwokozi mbarikiwa,
> Ninato-. . .

384 Sasa, ninyi mlio madhabahuni, kama kweli mnajitolea, mwinulieni Yeye mkono, muimbe, "Natoa yote. Natoa madhehebu. Natoa madhehebu. Natoa kanisa. Najitoa mwenyewe. Ninaacha wazo langu. Yote Kwako, Ee Mwokozi wangu mbarikiwa, ninatoa yote. Kwako, Mwo-. . . "

Ninatoa yote,
Ninatoa yote.
Yote Kwako, Ee Mwokozi mbarikiwa,
Nininatoa yote.

Kweli unamaanisha jambo hilo?

Ninatoa yote,

[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

385 Ninyi sasa hapa madhabahuni. Ninyi mlio hapa madhabahuni, ambao mmeomba. Kanisa limewaombea. Mliomba, ninyi wenyewe. Sasa kuna njia moja tu mnayoweza kuokolewa, hiyo ni, "Kwa imani mmeokolewa, na hiyo ni kwa njia ya neema." Neema ya Mungu ilizungumza na wewe, ikakuleta madhabahuni. Unaomba baraka za Mungu. Unataka Neno Lake. Unamtaka Roho Mtakatifu. Unataka fadhila za Mungu. Na kama unamtaka, na unaweza, kweli, kwa moyo wako wote, usalimishe. Sasa, usitafute mhemuko wowote. Tafuta Kweli, Kweli inayotoka moyoni mwako, kwa imani. "Bwana, niko tayari kufanya jambo lolote ambalo Neno Lako linaniamuru kufanya. Ninajisalimisha, kwa yote yaliyo ndani yangu."

386 Kama unaamini jambo hilo kwa moyo wako wote, ninataka usimame kwa miguu yako, uligeukie kanisa hili, wasikilizaji, na kuinua mikono yako juu, nasi tutauimba pamoja nao, "Natoa yote yaliyo ndani yangu, Mungu. Kadiri nijuavyo mimi, yote niliyo mimi, nayasalimisha."

387 Pandeni hapa kwenye jukwaa hili hapa, ninyi mliopo madhabahuni. Pandeni papa hapa jukwaani, enyi ndugu, papa hapa, ninyi nyote, na ndugu na dada.

Angalieni hapa, enyi kanisa.

388 [Dada fulani anasema, "Ndugu Branham, mimi ni mfuasi wa kanisa, bali hivi majuzi mimi siko—siko ndani yake tena."—Mh.] Umeliacha? ["Bwana anajua mahali ninapotaka kuongozwa Naye. Ninataka . . .?. . . kanisani. Na ninataka Roho Mtakatifu, kujazwa na Roho. Na ni afadhali nife, kama hilo ndilo linalohitajika."] Naam. Hiyo ni kweli. Je! unasalimisha kila kitu Kwake na kwa Neno Lake?

389 Dada mmoja hapa, kutoka katika madhehebu fulani. Alisema, "Mimi ni mfuasi wa dhehebu fulani." Hatuna haja ya kulitaja. Yeye ni mfanyakazi kule. Lakini alisema, "Ndugu Branham, ninataka kutoka niingie kwenye ile Kweli. Ninataka kitu fulani kilicho na kilindi zaidi kuliko hilo." Unaona?

390 Hebu nilinukuu Neno Lake. "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa."

391 Sasa, ninyi mlio hapa jukwaani, ambao mmekuja sasa hivi, kama mko tayari kuachana na yote mliyo, kila kitu, kulitii Neno la Mungu. Hakuna mtu aliyewaambia, juma hili, la kufanya. Sasa, kama mko tayari kujisalimisha sasa hivi Kwake, inueni tu mikono yenu, namna *hii*, kwa wasikilizaji. Sasa, ninyi mlio hapa jukwaani, hebu na tuuimbe pamoja sasa, *Ninatoa Yote*. Kila mtu, pamoja. Vema.

> Ninatoa yote,

Sasa kweli unamaanisha jambo hilo! . . . ? . . .

392 Je! kweli mnamaanisha jambo hilo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Semeni, "Amina," mara nyingine. ["Amina."] Semeni, "Bwana," ["Bwana,"] "nichunguze." ["nichunguze,"] "Nijaribu." ["Nijaribu."] "Na unipe nafasi." ["Na unipe nafasi."] "Haya ndiyo yote ningaliweza kufanya, usiku wa leo," ["Haya ndiyo yote ningaliweza kufanya, usiku wa leo,"] "ni kujitoa Kwako." ["ni kujitoa Kwako."] "Unajua njaa ya moyo wangu." ["Unajua njaa ya moyo wangu."] "Unajua shauku yangu." ["Unajua shauku yangu."] "Ahadi Yako ilikuwa ni kutimiza shauku hiyo." ["Ahadi Yako ilikuwa ni kutimiza shauku hiyo."] "Sasa naikubali." ["Sasa naikubali."] "Nami najitolea Kwako." ["Nami najitolea Kwako."] Wote pamoja.

> Ninatoa yote,
> Ninatoa yote.
> Yote Kwako, Ee Mwokozi mbarikiwa,
> Ninatoa yote.

*Muungano Usioonekana Wa Bibi-Arusi Wa Kristo* SWA65-1125
(The Invisible Union Of The Bride Of Christ)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 25 Novemba, 1965, katika Maskani ya Uzima huko Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org